

HESHIMA

 Hadi muda mfupi uliopita nilipoondoka hospitalini, na kwa namna fulani nililiacha katika mikono ya Bwana, kwamba kama—kama... nikijua nilikuwa kidogo nimepwelewa na sauti, sababu nina mafua. Lakini nilifikiri kama niki... kama mama angekuwa mzima vya kutosha basi ningeweza kuja, mbona, ningeshuka tena nije niwatembelee ninyi. Kwa sababu, ninapomwona mtu kama mamangu amelala pale na kujua kwamba hawa mama wengine na baba hapa, kwamba yatupasa sote kufikia mahali hapo, unaona, na kufikiria jinsi nilivyo na shukurani kwamba yeye yuko tayari kuaga dunia.

² Na halafu, ninataka kulielezea kanisa jambo jingine. Ninaamini nimenwona Dada Wilson nyuma kule. Na—na halafu yupo Dada na Ndugu Sothman hapa mahali fulani, labda, humu jengoni. Na—na wengi wenu hapa ambao mmekuwa mkitoa msaada wenu kukaa na mama usiku, na mambo kama hayo, huko ni kujitolea kabisa. Nami nashukuru kwa yote ninyi nyote mmetenda. Kwa kweli, jamaa yangu imechoka sana, mnajua, tunakesha kila usiku. Na sasa hivi tu, wengi wao hufanya kazi, kwa hiyo ni mimi na Meda, au—au Deloras, naye ana watoto shuleni, na kwa namna fulani ni vigumu kushika zamu kati yetu tukiwa wachache hivyo, nawe unachoka tu. Unaishi katika dhiki, na huwezi kutofautisha mchana na usiku, ni vigumu, hasa unapofikia kwenye umri tulio nao mimi na Meda, unajua, hai—haihitaji siku nyingi kukuchosha unapozeeka kidogo.

³ Kwa hiyo, nilizoea kufikiria ningeweza kukaa mchana na usiku. Ninge kuja kutoka California katika Ford yangu kuukuu ya muundo wa T, nami ningepata usingizi kidogo njiani, ikanichukua kama siku nne au tano, pengine siku saba, kufika. Na ningendesha gari, mchana na usiku. Nami ningechoka kidogo, nikatupa blanketi yangu chini ya gari, nikaingia mbugani, nikalala kwa masaa machache kisha nikaendelea. Nimebadilika sana tangu wakati huo, Ndugu Neville. Nimetambua tu kwamba nimepita umri wa miaka ishirini na mitano, unaona.

⁴ Na kwa hiyo ni—ni majaliwa kuwepo hapa nyumbani mwa Bwana usiku wa leo. Na asubuhi hii nilikuwa na ma—madogo, maandishi machache hapa ambayo nilitaka, ambayo Bwana alinipa. Nami niliwaza kwamba labda asubuhi hii, kama nikipata nafasi, ningelizungumzia jambo hilo kabla ya kufanya maombi ya wagonjwa. Lakini kwa kuwa tulikuwa tumechelewa katika yale maswali asubuhi hii, nilifikiria pengine kama mama angepata nafuu, basi pengine ingekuwa ishara kwamba ningeshuka kuja huku tena usiku wa leo, pengine,

na ningezungumza kidogo usiku wa leo kama lisingeingilia utaratibu wa Ndugu Neville mahali fulani.

⁵ Nami nikiwa nimesimama chumbani ndio tu nilisikia ushuhuda mzuri sana kuhusu dada fulani Mkristo ambaye yupo pamoja nasi usiku wa leo. Alikuwa katika mstari wa maombi asubuhi ya leo, na akaomba, akisimama kwa ajili ya mtu mwingine. Na chumbani mwake, chumba chenye giza, kuna *Ile—Meza Ya Bwana, Meza Ya Bwana Ya Mwisho*. Na kiko hivi kwamba jua haliwezi kupenya ndani ya chumba upande wo wote. Na wakati wa saa tisa alasiri ya leo, hii Duara ya Nuru ambayo ilionekana hapa tulipomaliza kuhubiri juu ya Nyakati za Kanisa, ikiwa tu katika rangi kama ya upinde wa mvua, namna hiyo, ilikuja moja kwa moja juu ya kichwa cha Bwana Yesu. Vema, aliitazama Hiyo muda mfupi. Naye akaenda akamwambia dada yake, namna ninavyoelewa hadithi ile, nao—nao wakaja na kuistaajabia kwa muda mrefu, saa moja ama kitu kama hicho. Na halafu walimwita jirani, mhudumu, ambaye ni Ndugu Stricker hapa, kuona tukio hilo la ajabu. Nao waliketi wakaiangalia, wakaendelea hadi saa kumi na moja au kitu kama hicho. Na yule mhudumu aliombwa kuomba, naye akajisikia kwamba hakuweza kuomba hata, au kitu kama hicho.

⁶ Punde si punde, mtu fulani alitoa ujumbe, (nao walikuwa wakitoa tafsiri ya maana yake), na ujumbe ukarudi, kwa kunena katika ujumbe ule, ukasema kwamba walikuwa “wameufasiri vibaya,” hawakuwa wameutoa sawa. Nafikiri hilo ni sawa, sivyo, Dada Bruce? Hawakuufasiri sawa. Kasema kwamba kusudi la ishara ile, ilikuwa kuwaonyesha, kama kwamba anapendezwa nao, kwa kuwa wameamini Ujumbe unaotoka hapa Maskanini, namna hiyo. Na kasema wataona mambo makubwa zaidi ya haya yakitokea, kwamba wangeona hata Malaika wakipanda, na kushuka na kupanda.

⁷ Kwa hiyo tunaishi katika siku za mwisho, na tuko karibu na wakati wa mwisho. Na mimi... Hili linasikika, laweza lisikike la kutisha kwa baadhi ya watu isipokuwa kwa Wakristo, ninafurahi kwamba tumefikia hapa. Ni—ninafuraha kwamba tuko mwishoni.

⁸ Nilisema hilo wakati mmoja mkutanoni. Na mtu aliyekuwa akizungumza nami, kasema, “Unamaanisha nini? Unamaanisha ungefurahi kuona mwisho wa ulimwengu ukifika?”

Nikasema, “Ah, ndiyo, bwana!” Nikasema, “Bila shaka!”

⁹ Kasema, “Vema, hilo si jambo la hekima, mtu kutaka mwisho wa ulimwengu uje?”

¹⁰ Nikasema, “Mwisho wa ulimwengu, wakati huo, Yesu yuaja, na Huyu Ndiye ninayetaka kumwona.” Ndipo nikasema, “Biblia ilisema hivyo, ‘Wale wote wanaopenda kufunuliwa Kwake!’ Unaona?”

¹¹ Na ni furaha kujua kwamba, kwamba mambo haya ya kale hapa ya maisha yatakoma hivi karibuni, na tuta—tutamwona Yeye.

¹² Lakini hivi majuzi, ilinenwa kule chini katika ile... Ah, miaka mingi kule nyuma, walipokuwa na utumwa. Na kulikuwa na m—mzee mweusi ambaye alikuwa... aliyependelea kuimba nyimbo za kale za kanisa, nyimbo za mashambani. Wangekusanyika pamoja na kuhudumu miongoni mwa watumwa, na kuhubiri, unajua, na kuendesha mikutano. Na usiku mmoja kulikuwa na mzee mmoja kule aliyeokoka. Naye alipookoka, hapo alijua basi alikuwa huru. Kwa hiyo akaanza kuwaambia wale watumwa wengine, asubuhi ya siku iliyofuatia huko shambani, akasema, “Niko huru.”

¹³ Kwa hiyo bosi wake akaja akamvuta akamwingiza ndani, akasema, “Sasa, angalia hapa, Sam.” Kasema, “Ni nini hiki ninachosikia unazungumzia miongoni mwa watumwa, kwamba wewe uko huru?”

¹⁴ Akasema, “Ndiyo, bosi.” Kasema, “Hiyo ni kweli.” Kasema, “Kwenye mkutano jana usiku, niliwekwa huru kutoka sheria ya dhambi na mauti.” Basi. Basi.

¹⁵ Sheria ya dhambi na mauti, niliwekwa huru nayo. Kwanza ulikuwa umefungiwa mle, unaona, lakini sasa uko huru. Unaona? Kama nilivyosema asubuhi hii, mauti hudumu tu katika dhambi. Dhambi na mauti ni sawa, unaona. Lakini unapokuwa umeondoka kwenye dhambi, umetoka katika mauti; lakini unapokuwa ndani ya dhambi, umo katika mauti. Unaona? Na kwa hiyo wakati uko huru kutoka sheria ya dhambi na mauti, wewe ni kiumbe kipya katika Kristo Yesu, ndipo uko huru.

¹⁶ Naye bosi wake akamwambia, akasema, “Sam, hivi kweli unamaanisha hivyo?”

¹⁷ Akasema, “Ndiyo, bwana.” Akasema, “Bwana aliniita usiku wa jana kuzungumza na watu wangu, nikawaambie, kwamba wanaweza kuwa huru kutoka sheria ya dhambi na mauti. Ingawa tu watumwa, lakini tunaweza kuwa huru kutoka sheria ya dhambi na mauti.”

Akasema, “Sam, kweli unamaanisha hilo?”

¹⁸ Akasema, “Bosi, sijui utanifanyaje nikisha kusema jambo hili, lakini mimi, mimi ninakuambia, mimi ni mtu huru.” Akasema, “Mimi ni huru kutoka sheria ya dhambi na mauti.”

¹⁹ Naye akasema, “Sam, mimi ni Mkristo, pia, unajua. Na kwa sababu wewe... Mungu amekuweka huru kutoka katika dhambi na mauti, na wewe u Mkristo, nawe unajisikia unataka kuwaambia ndugu zako jambo hilo. Nitashuka kwenda huko asubuhi hii nikakuweke huru, na kutia sahihi tangazo. Na unaweza kuwa mtu huru, asiye fungwa na mtu ye yote, upate kuwahubiria Injili ndugu zako.”

20 Akasema mzee yule alihubiri kwa miaka mingi, mingi sana. Na wakati mmoja basi, baadaye, kama sisi sote tunavyofanya, tunafikia kikomo cha safari yetu. Na tufikapo mwisho wetu wa... njia yake, alipofikia kikomo, akashuka akaja. Naye akazirai, walisema, kwa labda, loo, masaa kadhaa. Na wengi wa ndugu zake wazungu wakaja kumtembelea. Na ilitokea kwamba palikuwepo na kundi la hao katika lile jengo alipoamka, alipopata fahamu. Akatazama huku na huko, akasema, “Mnataka kusema bado sijawasili kule?”

Nao wakasema, “Sam, umekuwa usingizini.”

21 Akasema, “La hashu.” Akasema, “Sikuwa nimelala.” Kasema, “Nilikuwa nimevuka ng’ambo ya pili.”

22 Mbona, wakasema, ndugu wahudumu wakasema, “Sam, tuambie uliona nini ng’ambo ya pili.”

23 Kasema, “Naam,” akasema, “nilienda nikaingia lango kuu jeupe la lulu,” akasema, “wakati nilipoingia mle,” kasema, “niliona Kiti cha Enzi, kisha nikamwona Yeye.” Akasema, “Huyu hapa akaja malaika, akasema, ‘Wewe ni Sam?’”

Akasema, “Ndiyo.”

24 Kasema, “Sam,” kasema, “hili hapa va—vazi na taji.” Kasema, “Umezipata hizi, Sam, kwa kazi kuu ulizozitenda duniani.”

25 Akasema, “Usinizungumzie kuhusu joho na taji kama tuzo.”

Akasema, “Ungetaka upewe tuzo gani?”

Akasema, “Niruhusu tu nimtazame Yeye kwa miaka elfu moja.”

26 Nafikiri sote tunajisikia jinsi hiyo, sivyo? Si—sitaki majoho yo yote na taji na majumba ya kifalme. Nataka tu kumtazama Yeye. Ningetaka tu kumtazama Yeye, Yeye tu, unajua. Usingetaka tu... Ningetaka kuushika mkono wako ninapofanya hivyo, Ndugu Neville. Tungeweza kufanya hivyo pamoja nanyi, Hebu, “Lifikirie, Ndugu Neville, jinsi tulivyokaa Maskanini, katika joto na baridi, na kadhalika. Lakini angalia hapa jambo tunaloangalia, Mwana wa Mungu aliye hai.” Je! lisingekuwa la kupendeza sana, kutazama tu na kuona sura Yake!

27 Mimi, mara mbili katika maisha yangu sasa, mara tatu, nimemwona Yeye katika ono. Yeye alionekana vile vile kila wakati. Lakini hakuna mchoraji ulimwenguni angeweza kuchora picha Yake. Wanaweza kuchora kitu kinachoweza kufanana Naye. Bali Yeye alionekana kama, kwangu mimi, Yeye ni Mtu Ambaye kama angelinena ulimwengu ungeliangamia, na hata hivyo ni mpole sana na wa kupendeza sana, kwamba hakuna hata... kuna sifa nyingi sana mle ambazo brashi ya mchoraji isingeweza kupipata. Nami hakika nataka kumwona Yeye siku moja, Binafsi.

²⁸ Na mara nyingi nimewaza wakati ningependa kumsikia Yeye alipoinua hiyo mikono ya thamani na kusema, “Njoni Kwangu.” Nione huo uso Wake mchovu na wa simanzi, Yeye alipokuwa amelegea na kuchoka sana kwa safari Yake, kasema, “Njoni Kwangu ninyi nyote msumbukao, na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu, kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo.” Ningelitaka kumsikia Yeye akisema hivyo. Sikuwa hapo siku ile. Sikuwa nimesimama na Petro, Yakobo, na Yohana. Bali natumaini nitasimama karibu nao katika siku ninapoweza kumsikia Yeye akisema, “Vema, mtumwa Wangu mwema na mwaminifu, sasa ingia katika furaha za Bwana.”

²⁹ Na kufikiria kwamba watu wale ambao walioandika Biblia hii, Paulo, Isaya, na Yeremia, na mitume wote, na wale ndugu wa thamani, po pote walipo sasa, po pote walipo sasa . . . Mungu yeye yule aliyewashughulikia, kuona vitu kabla na kuvianzisha, na kadhalika, na kuwapa vipawa vya Biblia, unabii na kunena kwa lugha, na ishara na maajabu, na kadhalika. Watu wao hao, po pote walipo hivi sasa, tutakuwa pamoja nao. Mungu yeye yule na jambo lile lile. Si “tunadhania hivyo” tena, tunajua hivyo sasa, unaona, kwa sababu Yeye kweli yupo na tunajua kwamba ndivyo ilivyo. Kwa hiyo si tungekuwa watu wenye furaha zaidi ya watu wote ulimwenguni? Je, tungetamani nini tena?

³⁰ Nilikuwa nikizungumza alasiri hii na mzee fulani, yapata, nafikiri alisema alikuwa na umri wa miaka themanini na minane au themanini na tisa, ambaye hivi karibuni amekuwa Mkristo. Nilimbatiza katika Jina la Yesu Kristo, wakati hakuwa na kitu ila suti yake ya kawaida ya Jumapili. Nilimpeleka majini. Nafikiri Ndugu Wood alimpatia suruali moja au kitu fulani, na tulimbatiza hapa katika maji. Naye aliniambia, alipokuwa mvulana . . . Ni tajiri kidogo sasa. Naye, alipokuwa mvulana, alisema jinsi alivyofanya kazi kwa dola thelathini kwa mwezi. Hakuo au cho chote kile mpaka alipokuwa mzee. Naye alisema jinsi alivyotamani wakati ambao atakuwa mzee ambapo haitampasa kuomba na kulala mitaani. Jinsi alivyochukua hela ndogo na vitu mbalimbali ambavyo aliweka akiba, akavitia kazini, na kwa kweli vilifanya kazi na kuongezeka na kuzaa. Na sasa huyo hapo sasa, mwenye umri wa miaka themanini na kitu, themanini na minane au themanini na tisa, nafikiri ndivyo alisema, karibu kabisa na tisini, bado anatembea, ameketi papa hapa kanisani asubuhi hii. Na halafu ameweka akiba ya kutosha hata haitamlazimu kuona wasiwasi. Kama akiishi miaka mingine mia moja, hangeona wasiwasi juu ya fehda na mambo kama hayo. Ndugu mwenye moyo mzuri, mcha Mungu, hutenda kila kitu kwa ajili ya Wakristo na mambo anayojua kutenda.

³¹ Ndipo nikasema, “Na juu ya yote hayo, ndugu yangu wa thamani, ulipokuwa ungali na umri wa miaka themanini na

minane au themanini na saba, Mungu, katika rehema Yake, aliunyosha mkono Wake akakupa Uzima wa Milele katika Makao ya Mbinguni.” Ungetaka nini tena kumalizia maisha? Ndiyo, bwana.

³² Na utajiri wote ambao tungeweza kuukusanya, mambo yote ambayo tungeweza kutenda duniani, haidhuru ni mambo gani, aliyotenda mtu, huna budi kufa na kuacha kila kitu.

Usiutamani utajiri usio na maana wa
ulimwengu huu,
Ambao huoza upesi sana,
Tumaini mambo ya Milele
Hayatapita kamwe!

³³ Hiyo ni kweli. *Shikilia Mkono Wa Mungu Usiobadilika.* Naupenda wimbo huo. Tulizoea kuuimba huo hapa maskanini sana.

Wakati umejaa mambo yapitayo upesi,
Hakuna cha duniani kitakachodumu.
Tumaini mambo ya Milele,
Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

³⁴ Mama yangu mzee amelala kule usiku wa leo. Kama ningelikuwa na dola milioni mia moja, ningetoa kila senti yake ili nizungumze naye kwa saa moja. Ningezitoe. Hakika. Vipi kama angalikuwa na dola milioni mia moja, zingemfaa nini sasa? Ha-zifai kitu, unaona. Vitu alivyo navyo, haachi hazina zo zote za duniani. Bali, anaacha neno hili, anamjua Bwana Yesu kama Mwokozi wake. Hilo ndilo jambo muhimu.

³⁵ Mbele ya jambo hili, mimi—sote na tujichunguze usiku wa leo. Hebu na tufikirie tu kabla ya kuanza maombi, “Ukoje m—msimamo wangu usiku wa leo na Mungu?” Hebuni tuchunguze mioyoni mwetu tuone. “Bwana, kama nimemjeruhi mtu ye yote leo, kama nimesababisha mguu mmoja kupotea, cho chote ambacho nimefanya au kusema ambacho ni kosa, Ee Mungu, nisamehe.” Unaona? Hebu . . .

Imani yangu inaelekezwa Kwako,
Ewe Mwana-Kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Sasa nisikie ninapoomba,
Ondoa hatia zangu,
Na unijalie tangu sasa,
Kuwa Wako kabisa.

Huku nikizunguka mizingo yenye giza ya
maisha,
Na huzuni inatandaa kunizunguka,
Naomba uwe Kiongozi Wangu;

Agiza giza liwe mchana,
Nifute majonzi na hofu,
Wala usiniache nikatoka
Karibu Nawe.

³⁶ Nidumishe katika njia, Bwana. Niweke katikati ya mapenzi Yako. Vijana kwa wazee, hatujui unaweza kuwa na umri gani, na hata hivyo unaweza ukawa na umri wa miaka themanini, na kama ungeishi hadi asubuhi, ungeishi zaidi ya wavulana na wasichana wengi wenye umri wa miaka kumi na sita. Kutakuwa na wavulana na wasichana wengi wenye umri wa miaka kumi na sita watakaokwenda kukutana na Mungu kabla ya mapambazuko asubuhi. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo umri hausiani na jambo hilo. Jambo lenyewe ni kwamba, je, uko tayari kumlaki Yeye? Hilo ndilo jambo muhimu.

³⁷ Hebu na tuyafikirie mambo haya sasa tunapoomba, huku tumeinamisha vichwa vyetu.

³⁸ Ee Baba mwenye Neema na Mtakatifu, uliye Mtukufu na wa Uzima, twaja katika Uwepo Wako, Mungu Mwenyezi, kutoa shukurani kutoka katika vilindi vya mioyo yetu, kwamba tuna majaliwa ya kuketi hapa usiku wa leo. Nikitembea juu na chini kwenye ile hospitali muda mfupi uliopita, na nikiangalia mle ndani, kukiweko watu waliozirai, baadhi yao wakitokwa na damu na kulia, na wengine wamerukwa na akili na wamefungiliwa kitandani, Ee Mungu, ninaomba kwamba kila mmoja wao yuko tayari, Baba, kwamba wangukuwa tayari kukutana Nawe iwapo wataondoka katika maisha haya. Pia kufikiria, Bwana, kwamba hao waweza kuwa ni sisi, kila mmoja wetu hapa, kama si kwa neema Yako. Lakini umeturuhusu tuishi ili tukusanyike pamoja tena usiku wa leo, kufanya matayarisho. Mambo hayo yanapita miyoni mwetu na bongoni sasa, Bwana. Na wakati Wewe unachunguza viuno vya mioyo yetu, kama tuna jambo lo lote lisilo safi, Bwana, liondoe, Baba. Mungu, zitakase nafsi zetu Kwako.

³⁹ Tunakushukuru Wewe kwa yote yale Wewe umetenda na kwa yale tunayoamini kwamba Wewe utatenda. Na kwa Nuru ile iliyotokea leo chini kule katika nyumba ya Dada Bruce, ninakushukuru Wewe kwa ajili yake, Bwana, Jambo hilo litawapa nguvu.

⁴⁰ Na sasa, Bwana, ninaomba kwamba Wewe utatujalia usiku huu kwamba nafsi zetu ziendeleo kuburudishwa katika Uwepo Wako hapa katika Maskani haya. Tunakushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya Maskani haya. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya mchungaji wake hapa, Ndugu yetu Neville, mtu mnyenyekevu, mtu wa haki, mtu ambaye amejaa upendo wa Mungu kwa ajili ya Kristo na kwa ajili ya Kanisa Lake. Naomba kwamba Wewe utambariki pamoja na maskini mwenzi wake mzuri na watoto wake. Pia, Bwana, jalia waishi muda mrefu miongoni mwetu

hapa duniani. Tujalie. Walinde na maradhi nyumbani mwao na uwape afya. Kinga nyumba zetu zote na maradhi, Bwana, tupe afya ili tuweze kukutumikia Wewe.

⁴¹ Na sasa tunaziweka nafsi zetu juu ya madhabahu, kwa uchunguzi sasa, ninapofungua macho yangu hivi punde kusoma Neno Lako, kama ni mapenzi Yako, na kwa kuwa ni zamu yangu usiku wa leo kujaribu kumega Mkate wa Uzima kwa watu. Sasa, Bwana, nisaidie kusema kitu fulani ambacho kingesaidia maskini watu fulani wachovu hapa usiku huu. Jalia yawe pia ni maneno ya kusahihisha, tupate kujua jinsi inavyotubidi kuenenda sisi wenyewe, tujue la kufanya na jinsi ya kuishi katika ulimwengu huu wa sasa, kama tunatarajia kuifanya Mbinguni Makao yetu. Lijalie, Bwana. Na uyaponye maradhi. Kama kuna ye yote miongoni mwetu, Bwana, ambaye ni mgonjwa, tunaomba kwamba Wewe utauponya. Watie nguvu waliochoka. Tunawaombea.

⁴² Tunaomba si kwa ajili ya kanisa hili tu, lakini kwa ajili ya makanisa mengine ulimwenguni kote ambako maombi yanafanyika, na sala mbele za Mungu, na wengi wa makumi elfu ya watakatifu walio na mioyo yenye njaa na waliao, "Njoo, Bwana Yesu, njoo!" Loo, hakika Wewe utasikia kilio chetu, Bwana, siku moja, na utakuja.

⁴³ Kama ni zamu yetu kulala usingizi kabla ya hayo kutokea, kabla ya kule Kuja, tunajua kwamba tarumbeta italia nao waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza. Tutafufuka na kusimama kwenye Uwepo Wako siku moja. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hili, nasi tunaongojea wakati huo, na sasa iandae mioyo yetu. Kwani tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

⁴⁴ Sasa, sitazamii kuzungumza kirefu usiku wa leo, pengine dakika thelathini, au arobaini, kuhusu somo dogo hapa, ambapo ningetaka kwanza kusoma Andiko linalopatikana katika Kitabu cha Zaburi. Zaburi 105, na kuendelea kusoma hadi aya ya 15, hiyo ikiwemo. Ninaposoma zaburi hii, nataka msikilize kwa makini sana kusomwa kwa Neno, kwa sababu Neno la Mungu halitashindwa kamwe.

Mshukuruni BWANA, liitieni jina lake,

Wajulisheni watu matendo yake.

Sasa fikiria tu hilo!

Mshukuruni BWANA, liitieni jina lake,

Wajulisheni watu tendo lake.

Mwimbieni, mwimbieni kwa zaburi,

Zitafakarini . . . ajabu zake zote.

Jisifuni kwa jina lake takatifu,

Na ufurahi mioyo ya hao wamtafutao BWANA.

*Mtakeni BWANA na nguvu zake,
 Utafuteni uso wake sikuzote.
 Zikumbukeni ajabu zake ambazo amezifanya,
 Miujiza yake na hukumu ya kinywa chake.
 Enyi wazao wa Ibrahimu, mtumishi wake;
 Enyi wana wa Yakobo, wateule wake.
 Yeye, BWANA, ndiye Mungu wetu;
 Duniani mwote mna hukumu zake.
 Analikumbuka agano lake milele;
 Neno lile aliloviamuru vizazi elfu.
 Agano alilolifanya na Ibrahimu,
 Na uapo wake kwa Isaka.
 Alilomthibitishia Yakobo liwe amri,
 Na Israeli liwe agano la milele.
 Akasema, Nitakupa wewe nchi ya Kanaani,
 Iwe urithi wenu mliopimiwa.
 Walipokuwa ambao . . . Walipokuwa—watu wawezao
 kuhesabiwa,
 Naam, watu wachache na wageni ndani yake,
 Wakatangatanga kutoka taifa hata taifa,
 Toka ufalme mmoja hata kwa watu . . .
 Hakumwacha mtu awaonee,
 Hata wafalme aliwakemea kwa ajili yao.
 Akisema, Msiwaguse masihi wangu,
 Wala msiwadhuru nabii zangu.*

⁴⁵ Nataka kuchukua somo toka hapo, la: *Heshima*. Ukisoma hapa, Daudi akimlilia Bwana. Heshima ndiyo tunayowiwa na Mungu. Na hilo ni jambo moja ambalo ningetaka, kulishindilia ndani ya moyo wa kila mtu hapa usiku wa leo, kwamba, katika mambo yote ambayo tunaona yakiendelea, yatubidi tuyaheshimu. Unaona, yatubidi tuyaheshimu. Na Daudi alisema kwamba walipokuwa watu wachache sana wa Israeli, pengine Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, ambao alikuwa akizungumza habari zao, watu wachache sana, kwamba Yeye alikemea mataifa na wafalme kwa ajili yao. Mungu aliyakemea mataifa na wafalme, akisema, “Msiwaguse masihi Wangu, wala msiwadhuru nabii Wangu.”

⁴⁶ Katika Mhubiri, sura ya 12 na aya ya 13, imeandikwa hivi, unaona.

*Hii ndiyo jumla ya maneno, yote yamekwisha sikiwa;
 Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake,*

Maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu.

⁴⁷ Jumla ya maneno ni “mche Mungu.” Na, basi, huwezi kuwa na heshima mpaka uwe na kicho. Yakubidi uwe na kicho cha Mungu. Sulemani alisema pia, katika Mithali, kwamba;

Kumcha Mungu ni chanzo cha hekima;

Kumcha Mungu ni chanzo cha hekima;

⁴⁸ Sasa, hilo halimaanishi kwamba unamwogopa Yeye, bali hilo humaanisha kwamba unampa “heshima” na “kicho.” Na unapomheshimu Mungu, unamcha Mungu. Unaogopa kwamba unaweza umuudhi Yeye kwa njia fulani, unaogopa usije ukafanya makosa. Hungetaka kuyatenda.

⁴⁹ Namheshimu mama yangu. Namheshimu m—mke wangu. Naliheshimu kanisa langu. Nawaheshimu watumishi wote wa Mungu, nisije nikaweka jiwe la kujikwaza mahali fulani njiani mwao. Na—nawaheshimu watu. Nawaheshimu watu wa mji, nisije nikatenda jambo baya ambalo litawafanya kufikiri kwamba sikuwa Mkristo.

⁵⁰ Unaona, yakubidi, kabla ya kuwa na heshima, yakubidi kuwa na kicho. Na Mungu huidai hiyo, Yeye anadai heshima. Mungu anadai, Yeye huidai. Nacho kicho ndicho kinachoileta. Na tunajua kwamba kicho huleta heshima.

⁵¹ Sasa, chukua kwa mfano, mtu, yeye ni mkulima au pengine yeye ni—muuza duka, na hakuna anayemjali. Lakini hebu na apate kazi katika jeshi la polisi na ashuke aje barabarani, na kama po—polisi akiwa amevaa beji na nguo rasmi (ambapo, pengine mtu fulani asingezungumza naye siku moja kabla). “Jambo, ewe Yohana! U hali gani?” Unaona? Mbona hivyo? Ni namna fulani ya hofu, au woga, au staha, kwa sababu ya jambo hilo. Pengine achaguliwa kuwa meya wa jiji, au pengine . . .

⁵² Raisi Kennedy angekuwa nani usiku wa leo, kama asingekuwa Rais Kennedy? Vipi kama angekuwa mtu yule yule, lakini hata hivyo awe mfanya kazi ambaye anafanya kazi katika Colgates chini hapa kwa dola arobaini kwa juma? Unaona? Angekuja apitie mjini hapa na hakuna mtu angelimjali, ila wanaoshirikiana naye. Lakini, kwa kuwa yeye ni Raisi wa Marekani, anastahili heshima, unaona.

⁵³ Na kwamba, na kwa kuwa Mungu ni Mungu, Yeye anastahili heshima. Hiyo ni kweli. Na Yeye, yatubidi kumheshimu Yeye. Na kumpa Yeye uchaji, nao huo huleta heshima. Mungu amedai jambo hilo kwa ajili Yake Mwenyewe na kwa watumishi Wake wote. Mungu anadai heshima kwa ajili ya watumishi Wake. Yeye, watumishi Wake, vile tunavyojua kwamba hao ni watumishi Wake, ni kwa sababu Yeye huwathibitisha hawa watumishi kwa Neno Lake. Yeye huwachukua watumishi hawa na kuwafanya watumishi wa Mungu, Naye akathibitisha kwamba hao ni watumishi, kwa kulifanya Neno Lake litende

kazi kupitia hao watumishi. Basi unapomheshimu mtumishi yule, unamheshimu Mungu. Kwa hiyo ninapokuheshimu wewe na wewe unaniheshimu mimi, nasi tunaheshimiana, basi tunamheshimu Mungu.

⁵⁴ Je, Yesu hakusema, “Kadiri mlivyomtendea mmojawapo wa hawa walio wadogo, watoto Wangu, mlinitendea Mimi. Na ingefaa ufungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia na kutoswa katika kilindi cha bahari, kuliko kumkosesha mmoja wao. Kwa maana nawaambia, wanaangalia nyuso zao, malaika zao sikuzote huutazama uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni.” Sasa, tunajua kwamba wao ndivyo walivyo, kwamba sisi, tukiwa watoto wa Mungu, kwamba tu sehemu ya Mungu. Na Mungu anadai heshima hii. Na halafu Mungu huonyesha watoto Wake ni akina nani. Yeye—Yeye huonyesha kwa maajabu na ishara, na kwamba jambo hilo linatendeka.

⁵⁵ Sasa, tutaanza sasa kuzungumza juu ya baadhi ya watu hawa. Sasa, kama nitasema, mmoja wao, kwanza, ambaye ningefikiria habari za—zake... Hebu tumchukue Nuhu, kidogo. Sasa, Nuhu alikuwa na ufunuo kutoka kwa Mungu, hata hivyo ulikuwa kinyume cha cho chote ambacho sayansi ingethibitisha kuwa kweli. Lakini hata hivyo alizungumza na Mungu, na Mungu alikuwa amezungumza naye. Naye aliendelea kujenga safina. Ambapo, wenye dhihaka na wenye mizaha, kama Biblia ilivyosema kwamba wangelikuwa katika siku za mwisho kama vile walivyokuwa katika siku hizo, kwamba hao wenye dhihaka walimdhihaki Nuhu. Mbona, walifikiria kwamba yeye ni mwenda wazimu kwa sababu alikuwa anajenga safina. Kwa hiyo, lakini Mungu alileta hukumu juu ya hao wenye dhihaka, kwa sababu wasingemsikiliza mjumbe wa Mungu na kuingia safinani chini ya mahubiri yake, basi Mungu akatuma hukumu Zake duniani. Kwanza Yeye alifanya matayarisho kwa wote ambao wangelipokea, kuikimbia, na halafu kama hawakuikimbia, kuna jambo moja tu lililobakia. Kama hawayakubali matayarisho ya Mungu ya kuponea, basi kuna kitu kimoja tu kilichobakia, hiyo ni hukumu ya Mungu.

⁵⁶ Unaweza tu kufanya mambo mawili, aidha rehema ama hukumu. Yakubidi ukubali moja au jingine. Hapo ndipo tunaposimama usiku wa leo. Ama tunapokea rehema ya Mungu ama tunakabili hukumu Yake. Hakuna njia ya kuliepuka. Mungu sikuzote hutengeneza njia ya kuepukia kwa wale wanaotamani kuepuka. Halafu Yeye ana... Kilichobakia, yabidi kisimame hukumuni. Si kwa sababu Mungu anawataka kusimama hukumuni, bali kwa sababu wamechagua njia hiyo wenyewe. Unaona, wanajichagulia wenyewe. Hapo ndipo tunaposimama usiku wa leo, marafiki, jambo lile lile. Tunaweza aidha kuchukua njia ya Mungu ya kuepukia, ama twaweza kuzikabili hukumu Zake, lo lote tunalotaka kutenda. Hivi hufurahii usiku wa leo kwamba umekubali njia ya kuepukia? Kwa sababu, wote

ambao wanakataa njia ya kuepukia, itawapasa waje chini ya hukumu.

⁵⁷ Halafu kuna mtu mwingine ningetaka kuzungumza habari zake. Kulikuwa na nabii mkuu na mwenye nguvu jina lake Musa. Watu (Israeli) walipaswa kuelewa, kulingana na Maandiko, kwamba Mungu alikuwa anataka kuwakomboa na alikuwa anataka kuwatoa Misri. Bali mara tu Mungu alipomtayarisha mtu Wake na kumpeleka chini huko Misri, hawakumheshimu. Walimfukuza, wakasema, “Je! wataka kutuua sisi kama ulivyomuua yule Mmisri?” jambo ambalo liliwafanya wakae utumwani kwa miaka arobaini zaidi. Walikaa katika utumwa kwa sababu walikataa kumheshimu mkombozi ambaye amekuja kuwakomboa. Hilo liliwarudisha tena utumwani. Siyo kwa sababu ati Mungu aliwataka wakae, (wakati ulikuwa sawa kabisa), lakini kukaa miaka arobaini zaidi kwa sababu walikataa kukubali njia aliyoiweka Mungu ya kuepukia.

⁵⁸ Jinsi ninavyoamini kwamba hiyo ndiyo shida usiku wa leo. Jambo lile lile, unaona.

⁵⁹ Kwamba waliikataa njia ya kuepukia, na Mungu alikuwa ameazimia, na amekwisha kumwambia Ibrahimu na hao wengine katika agano Lake (kama tulivyosoma Daudi akiimba wimbo juu yake usiku wa leo). Yeye alikuwa amewaahidi kwamba angetenda jambo fulani, kwa hiyo Mungu atashika ahadi Yake. Yeye alikuwa anataka kuwatoa, kwa vyo vyote, lakini labda karibu kizazi kingine kilikufa. Kizazi kile cha zamani kilichomcheka Musa, na kadhalika, na hakingeukubali Ujumbe, kizazi kile (miaka arobaini) kilikufa, na Musa akaja kwenye kizazi kingine. Unaona ninachomaanisha? Kama hawaukubali, basi Mungu ataacha kizazi kile kipite na Yeye ataleta kizazi kingine kulitenda. Kwa hiyo, walikuwa wamelikataa. Na halafu tunaona, kizazi hiki kingine ambacho kilikuja, Musa aliposhuka kwenda kule kujithibitisha mwenyewe. . .

⁶⁰ Unajua, Musa aliogopa kushuka kwenda kule tena. Musa alikuwa na umri wa miaka themanini sasa, naye alikuwa hayupo kwa miaka arobaini. Naye alipozungumza na Mungu kwenye kijiti kilichowaka moto, alisema, “Nitawaambia ni Nani aliyenituma?” Mungu hakuwa na jina. Yeye akasema, “Nitawaambia nimetumwa na Nani?” Kasema, “Nitakaposema, ‘Mungu wa baba zenu amenitokea,’ watasema, ‘Ni nani huyo Mungu wa baba zetu?’ Naam, nitawaambia nini?”

⁶¹ Akasema, “Wewe waambie kwamba ‘MIMI NIKO AMBAYE NIKO.’ Wewe waambie kwamba ‘MIMI NIKO AMBAYE NIKO.’” Naye akasema, “Hiyo ni nini mkononi mwako, Musa?”

⁶² Akasema, “Fimbo.” Naye akaitupa chini ikageuka ikawa nyoka. Ndipo akaweka mkono wake kifuani mwake, ukageuka ukawa ukoma; akaurudisha, ukapona.

⁶³ Yeye akasema, “Shuka uende, ukazichukue ishara hizi na ukazitende mbele ya watu, na itakuwa thibitisho. Watajua kwa ishara hizi kwamba nimekutuma kwa ajili ya ukombozi.” Ee, ndugu! Mungu sikuzote hutenda jambo hilo. Mungu sikuzote hutoa ishara za kimbinguni. Unaona?

⁶⁴ Na sasa aliposhuka na kuwaita watu, na kutenda ishara zake mbele yao, Israeli yote iliamini, kila mmoja wao. Nao wakaenda moja kwa moja hata kwenye jumba la mfalme, pia, kwa ajili ya ukombozi. Ndipo Farao akaamua hatawaacha huru, basi Mungu akaachilia hukumu juu ya Farao. Nasi tunajua nini kilitukia huko Misri.

⁶⁵ Ajabu, baada ya kuona ishara zote zile zikitendeka, na halafu wakafika kwenye Bahari ya Shamu, na kuona kwamba Mungu yeye yule ambaye ametenda ishara zote zile, hapa kwenye Bahari ya Shamu, walimshuku Mungu, jambo la kwanza kabisa, kwamba Yeye aliweza kufanya mlango wa kutokea.

⁶⁶ Sasa, hapo ndipo ambapo tunafanya kosa letu. Ugonjwa mdogo unapotupata, wakati maafa kidogo, au matatizo kidogo yanapotupata mahali fulani njiani, ndipo tunaanza kuanguka. Mwongofu mchanga; mtu fulani atamdhihaki, aseme, “Naam, wewe hu cho chote ili mtakatifu anayefingirisha.”

⁶⁷ “Naam, ninachukia kuitwa mtakatifu anayefingirisha.” Unaona, unaona, basi, unaona hiyo shaka.

⁶⁸ Huo ndio wakati wa kusimama pale! Huo ndio wakati wa kumheshimu mjumbe. Huo ndio wakati wa ku—kumpa Mungu utukufu.

⁶⁹ Basi Musa akasema, “Nimekwisha yatenda haya tayari, miujiza kumi mbele yenu. Naye Mungu amewapa miujiza kumi, na halafu mnaogopa baharini. Hakika. Mnataka mingapi zaidi mpate kuamini?” Akarudi nyuma, akachukua fimbo yake na akaishikilia mbele ya bahari, basi tufani zikaja na kuipeperushia upande ule mwingine, nao wakavuka. Na mara tu walipofika kule, mara wakaanza kulalamika hawana mkate. Unaona, jambo lile lile tu. Ndipo Mungu akanyesha mkate kutoka mbinguni kwa ajili yao. Halafu wakalalamika hawana maji. Walikuwa na lalamiko moja baada ya jingine. Ndipo naona . . .

⁷⁰ Unasema, “Vema, pengine walikuwa namna ya watu wasioongoka.” Vema, pengine walikuwa hivyo. Kulikuwa na watu waliochangamana nao wakakwea pamoja nao, ni kweli.

⁷¹ Lakini nataka ku—kuwakumbusha jambo lingine. Kama Mungu alimtuma mjumbe, na akamdhihirisha, kwa ishara, kwamba yeye ni mjumbe aliyetumwa na Mungu, basi ni juu yao kumtii mjumbe huyu. Sawa kabisa. Yawabidi wamtii mjumbe yule na kumheshimu mjumbe yule. Waangalie Yoshua na Kalebu, walikaa moja kwa moja karibu naye. Ndiyo, bwana. Lo lote alilotenda Musa, waliliunga mkono, pia. Iwapo Musa alikuwa

sahihi au alikosea, walimuunga mkono, kwa vyo vyote, unaona, kwa sababu walijua huyo alikuwa mjumbe wa Mungu.

⁷² Na hapo siku moja tunaona kwamba hata Miriamu, nabii mke, na Haruni, kuhani mkuu, walimdhihaki mke wa Musa kwa sababu alikuwa Mkushi, wakafikiria, “Hawakuwepo wanawake wa kutosha wa kundi letu wenyewe, wa kuoa, badala ya kushuka kwenda chini kule na kumwoa mwanamke yule?” Hilo halikuwa chaguo la Musa; hilo lilikuwa chaguo la Mungu kwa Musa. Na walipolidhihaki, hilo lilimkasirisha Mungu sana hata Yeye akampiga Miriamu, yule nabii mke, akajaa ukoma, dada yake Musa. Na hilo je? Yeye, nabii mke, lakini alikuwa akifanya nini? Alikuwa akidhihaki na kutomheshimu mjumbe wa Mungu, mjumbe wa agano la siku ile. Hakuwa na heshima. Na pia Haruni, kuhani mkuu, aliye kweli mnenaji wa Musa, sawa, alikuwa pamoja na Miriamu.

⁷³ Na Haruni basi, alipomwona dada yake amepigwa na ukoma, aliingia akamwambia Musa, “Utamwacha dada yako afe?”

⁷⁴ Basi Musa akaingia maskanini akaanguka mbele za Bwana, akaanza kumlilia na kumwita Mungu, rehema kwa ajili ya dada yake. Ndipo Roho wa Bwana akashuka akasema, “Mwite Haruni na Miriamu wasimame hapa mbele Zangu.” Loo, jamani!

⁷⁵ Mungu hudai heshima! Mungu akiutuma Ujumbe Wake, usikize Huo na kuuheshimu Huo. Usijali kama watauita Huo tita la watakatifu wanaojifingirisha, au cho chote kile wanachouita Huo; acha walimwengu watende wanalotaka kutenda. Lakini wewe heshimu!

⁷⁶ Kwa hiyo, Miriamu alisimama pale. Mungu akasema, “Mwite Miriamu kisha umwite Musa... au mwite Haruni hapa, ndugu na dada yako, wasimame mbele Zangu.”

⁷⁷ Na wakati walipokuja mbele za Mungu, Mungu akasema, “Hivi hamumchi Mungu?” Kasema hayo kwa kuhani mkuu na kwa Miriamu nabii mke. Kasema, “Akiwepo ye yote, mtu miongoni mwenu, wa rohoni au nabii, Mimi Bwana nitajifunua Mwenyewe kwake. Nitasea naye katika maono na kujifunua Mwenyewe kwake katika ndoto, na kadhalika, kama yeye ni wa kiroho au nabii.” Lakini kasema, “Mtumishi Wangu Musa, Mimi huzungumza naye mdomo kwa sikio.” Kasema, “Hivi hamumchi Mungu?” Kwa maneno mengine, “Mkinena habari za Musa, mnaninena Mimi. Kama hamwezi kumheshimu Musa, hamniheshimu Mimi.” Kasema, “Je! sikuthibitisha miongoni mwenu kwamba yeye ni mtumishi Wangu? Nanyi hamna heshima kwake hata kidogo.”

⁷⁸ Hilo lingekuwa somo jinsi gani kwa watu wa siku hii, hawana heshima, hawana staha!

⁷⁹ Sasa Yeye akasema, “Na kwa sababu hukufanya jambo hilo, hiyo ndiyo sababu una ukoma. Hiyo ndiyo sababu mambo haya yamefanyika,” kasema, “kwa sababu ilikubidi kujua kwamba

huyu ni mtumishi Wangu. Mnalijua hilo, kwa hiyo mnaponena jambo dhidi yake mnalinena dhidi Yangu.”

⁸⁰ Kwa hiyo Musa akaomba kwamba maisha yake yahifadhiwe, Naye Mungu akayahifadhi maisha yake. Hakuishi kwa muda mrefu baadaye, akafa. Lakini alitakaswa ukoma wake, naye alitolewa nje ya kambi kwa siku saba, unajua, kwa—kwa ajili ya utakaso, kujitakasa na ukoma wake. Mungu alimponya.

⁸¹ Lakini kile ambacho Yeye alikuwa akijaribu kuwaambia, ni hiki, “Yakubidi kuheshimu nifanyacho Mimi.”

⁸² Na iwapo huo ndio uliokuwa msimamo wa Mungu katika siku ile, na Mungu hawezi kubadilika, Mungu anataka tuheshimu jambo analotenda. Yeye anadai jambo hilo. Kasema, “Au mtaliheshimu hilo au jambo lingine litatendeka.”

⁸³ Hivi majuzi mtu fulani aliniambia, alisema mimi... Mtu maskini, anafagia hapa sokoni, apate riziki. Alichanganyikiwa, yuko katika hali mbaya sana. Ni wa dini ya Kiluteri, na walikuwa na ushirika. Hajiwezi kabisa kwenda kanisani kwa miguu, kwa hiyo akachukua teksu. Kasema ilimgharimu senti themanini kushuka kwenda na senti themanini kurudi. Jirani yake, asiyemcha Mungu kabisa, alimwona akiomba Sala ya Bwana asubuhi moja, naye akamcheka, akamdhihaki. Akamwambia jirani yake, akamwambia mtu huyu, akasema, “Ulikwenda wapi na teksu asubuhi hii?”

Akasema, “Kulikuwa na ushirika. Nilishuka nikaenda kanisani.”

Akasema, “Ushirika ni nini?”

Akasema, “Tunaposhiriki mkate na divai.”

⁸⁴ Akasema, “Nilikuwa na wangu, pia, asubuhi hii mezani, na kipande cha mkate mwepesi na chupa ya wiske.” Unaona?

⁸⁵ Nawajua wavulana watatu wakati mmoja ambao walidhihaki ushirika kanisani, nawajua. Nao walikwenda kwenye—kwenye chumba cha hoteli na wakala sambusa ya nyama ya nguruwe na chupa ya wiske, nao wakafanya ushirika wao juu kule, wakidhihaki ushirika waliokuwa nao katika kanisa la Kipentekoste. Haikupita miezi mitatu tokea hapo, wote watatu walikuwa... mmoja wao alikuwa amekufa, na wawili walikuwa katika hospitali ya wenda wazimu.

⁸⁶ Huwezi kumvunjia Mungu heshima! Yakubidi kumheshimu Mungu. Kama huliamini, nyamaza tu, liache. Au, aidha fanya hivyo, au njoo kwa kicho sana na uheshimu jambo hilo. Usiwadhihaki watu walio katika Roho. Usiwanene watu ambao wanaabudu katika Roho wa Mungu. Waache.

⁸⁷ Nilikuwa nimesimama papo hapo pembeni, nikihubiri, miaka michache iliyopita, kama mhubiri kijana. Ndipo akaja mwanamke fulani, alikuwa wa dini ya Katoliki; lakini nilimjua mu—mumewe alikuwa Mkatoliki, naye hana dini.

Naye ni mwanamke mrembo sana, mwenye sura nzuri, anayependeza macho, mwenye umri wa miaka ishirini, ishirini na miwili. Nilimjua alipokuwa msichana hapa mjini. Naye akaja akasimama pale, kisha akasema, “Singemruhusu ng’ombe wangu nimpendaye afuate dini aliyi nayo William Branham.”

⁸⁸ Na usiku uliofuatia, kabla sijaweza kumfikia, nikasikia yuafa hospitalini, na bado sijui kilichomuua. Alikuwa mahututi sana kule hospitalini, naye mumewe akaja kunichukua. Akasema . . . Yeye alikuwa ni Mkatoliki. Naye akaja, akasema, “Njoo upesi ukaombe dua kwa ajili ya mke wangu, amekuwa akikuita jioni yote, anakufa.”

⁸⁹ Vema, nikasema, “Nitakwenda.” Ndipo nikaingia kwenye gari nikaondoka mkutanoni, nikaanza kwenda hospitalini. Basi nikapanda vipondio haraka, nikakutana na nesi, naye akasema, “Tayari amekwisha kufa.”

Basi akasema, “Njoo, sema sala kwa ajili yake, hata hivyo.”

Nikasema, “Amekufa.”

Kasema, “Sema sala, hata hivyo.”

“Haitawasaidia sasa.”

Kasema, “Vema, njoo umtazame.”

⁹⁰ Basi nikashuka nikaenda kule. Alikuwa na zile nywele nyekundu nyeusi, naamini wanaziita, nywele za hudhurungi. Mwanamke mrembo sana, madoa machache sana ya ngozi kwenye uso wake hapa, na macho makubwa mno ya kahawia. “Na mwanamke huyo,” nesi yule akasema, “Billy, alikufa katika maumivu mengi sana hata alitamka jina lako kwa nguvu sana na kwa sauti kubwa alivyoweza, akisema, ‘Mwambie anisamehe,’ mpaka yale madoa yalitokeza kwenye uso wake kama vivimbe.” Na yale macho makubwa yalitokeza na kope zake zimeyafunika nusu. Bila shaka, mnajua inakuwaje mtu anapokufa, figo zao na matumbo huchezacheza, na alikuwa pale akitoka mvuke kila mahali. Na alikufa katika maumivu makali sana kwa sababu . . . siyo kwa sababu hakuniheshimu mimi, lakini hakuiheshimu Injili ile niliyokuwa ninahubiri, na Mungu alikuwa akitenda ishara na maajabu.

⁹¹ Siku moja huko New Albany, nilipokuwa nimesimama pale nikizungumza na mwenye dhambi, nikimwongoza kwa Kristo, mzee mkubwa mkatili aliyekuwa katika gereji, mtu aliyekuwa rafiki yangu, mwana mkwe ana gereji iliyo jirani. Nilikuwa nimesimama pale nikihubiri wakati wa chakula cha mchana, nikila sambusa na kumzunguzia kuhusu Mungu. Mchana ningetafuta mahali fulani ambapo ningeweza kwenda wakati wa chakula cha mchana na kujaribu kumvuta mtu kwa Kristo. Akasema, “Bw. Branham,” kasema. Nilikuwa tu kijana mhubiri, mimi mwenyewe. Akasema, “Bw. Branham,” akasema,

“mama yangu alikuwa na dini kama hiyo, hiyo dini ya moyoni kabisa.” Na machozi yalikuwa yanamtiririka mashavuni.

Nikasema, “Ni muda gani tangu aage dunia?”

Akasema, “Miaka mingi. Sikuzote aliniombea.”

⁹² Nikasema, “Mungu aliyesikia maombi yake anajaribu kuyajibu sasa hivi kwa ajili yake.”

⁹³ Ndipo mtu huyu akaingia mle, akasema, “Aloo.” Alikuwa amelewa. Kasema, “We, Billy, sikiliza.” Kasema, “Wakati wo wote unaotaka kuja kwenye gereji yangu,” kasema, “njoo, lakini,” kasema, “usilete hiyo dini yako ya kale ya watakatifu wanaojifingirisha huko.”

⁹⁴ Nikageuka na kumtazama, nikasema, “Mahali po pote asipokaribishwa Kristo, sitakuwepo mimi.”

⁹⁵ Na kwa hiyo akageuka akasema, “Aa, jirudie, kijana.”

⁹⁶ Na nikasikia tu moyoni mwangu, Sauti ikisema, “Unavuna unachopanda. Yakufaa ufungiwe shingoni jiwe kubwa la kusagia, na kutoswa katika kilindi cha bahari.” Ndipo mwana mkwewe, alasiri ile ile, alimkanyaga na gari la aina ya Chevrolet la tani mbili lililojaa mizigo, akampondelea ardhini.

⁹⁷ Unaona, yakupasa kumheshimu Mungu. Yakubidi kumheshimu, wewe . . . Mungu anadai heshima, na Yeye anaidai.

⁹⁸ Na kwa hiyo Miriamu ilimpasa kujua vyema zaidi. Vile vile ilimbidi—ilimbidi Haruni kujua vyema zaidi, kuliko kujua hili, kwamba Musa aliongozwa na Roho wa Mungu kutenda ambalo alikuwa anatenda.

⁹⁹ Mhudumu wa Kibatisti aliniandikia barua siku chache zilizopita, kutoka hapa. Loo, kama hakunioka juu ya makaa! Akasema, “Mtu ambaye ni mvivu kama wewe! Huduma ambayo ingelingana na ya Eliya, manabii,” akasema, “na halafu kukuona umekaa nyumbani hufanyi lo lote!”

¹⁰⁰ Kwa hiyo Billy anashughulika kama katibu wakati ule, akamwandikia barua. Ndipo akawaza, “Naam, naamini nitamjibu tu,” akasema. Lakini akawaza afadhali anipatie niisome kabla ya kuijibu. Lakini ilikuwa ya kiungwana sana. Akasema, “Sasa, haya si ya baba yangu, haya ni yangu.” Kasema, “Ulisema sasa hivi kwamba baba alikuwa na huduma kama ile ya Eliya.” Kisha kasema, “Ulisema aliketi chini kwenye kijito kidogo mahali fulani, ameshika ndoana mkononi mwake, au milimani, ameshika bunduki mkononi mwake.” Akasema, “Utasema nini kuhusu Eliya wakati alipoketi miaka mitatu kando ya kijito?” Akasema, “Hivi hujui kwamba wanaongozwa na Roho wa Mungu kutenda ambalo wanatenda?” Unaona, kila mtu anataka kuiendesha namna yao. Lakini mtu lazima aongozwe na Roho wa Mungu, na lazima muiheshimu. Ni hilo tu.

¹⁰¹ Hapa hivi majuzi, mtu wa thamani, mjini hapa, alimwona ndugu mwingine, akasema, “Bill yuko wapi?”

Akasema, “Yuko huko Canada.”

Akasema, “Nadhani alienda kuwinda?”

Akasema, “Ndiyo, amekwenda kuwinda.”

Akasema, “Aa, upuzi kwa jambo kama hilo!”

¹⁰² Sawa, mtu yule, bila kujua kwamba nilikuwa chini ya uweza wa Roho Mtakatifu, kwa ono la BWANA ASEMA HIVI, kwenda. Utafanya nini siku ya Hukumu? Itanifaa nini mimi kwenda kwenye kitanda cha mtu yule na kumwombea? Kwanza, haniamini. Na watu, wanapokuja na kusema mambo haya, kana kwamba sijui kwamba hawaiamini? Ingawa wanakupigapiga mgongoni na kukuita “ndugu,” hata hivyo unajua hawaamini Hilo. Unaona? Hawaamini Hilo. Nawe unaweza kuwa . . . Huwezi ukawasaidia kwa jambo hata moja. Watakuita, “njoo uombe,” lakini haiwafai kitu. Kwa sababu, unaona, hawaiheshimu Hilo. Yakubidi kuliadini. Angalia wale ambao kweli wanaamini, na angalia nini kinatendeka. Unaona, yakubidi uheshimu jambo hilo.

¹⁰³ Yezebeli, katika siku za Eliya, jinsi alivyokosa kumheshimu Eliya! Jinsi yeye . . . Eliya kwa kweli alikuwa ndiye mchungaji wake. Hakika. Loo, hangepokea hilo. Masalale, hata! Yeye alikuwa—alikuwa asiyeamini kuna Mungu, au alikuwa kafiri au—au mwabudu sanamu. Naye alikuwa na makasisi wake wapagani. Lakini hata hivyo Eliya alikuwa ndiye mchungaji wake. Mungu alimpeleka yeye pale kuwa mchungaji. Alikuwa mchungaji kama . . . Kama alimkemea na kumwambia dhambi zake zote, hata hivyo alikuwa mchungaji wake. Yeye asingelipokea hilo kamwe, bali, naye alikosa kumheshimu. Alimchukia! Hakika, alimchukia! Na nini kilichompata? Mungu aliruhusu mbwa wamle barabarani. Hiyo ni kweli. Kwa sababu gani? Alikosa kuheshimu Ujumbe ambao Eliya alikuwa akihubiri.

¹⁰⁴ Mungu hudai heshima. Yakubidi uwe nayo. Ukitaka kupata cho chote kutoka kwa Mungu, itabidi umheshimu Mungu. Na yabidi ulitende kwa moyo wako, kilindi cha moyo wako. Lazima ufanye hivyo.

¹⁰⁵ Bali yeye alikosa kumheshimu Mungu alipokosa kumheshimu nabii Wake. Sasa, yeye alijua Eliya alikuwa ni nabii. Hawakuwa na cho chote katika Israeli kilichoweza kulinganishwa na Eliya. Mbona, maono yake na kila kitu vilikuwa vikamilifu mbele za Mungu. Naye, lakini aliwahukumu. Rehema, ndiyo! Angefikia kila madhehebu, kila kitu kingine. Na kila kitu kiitwacho dhambi, alikihukumu, tokea aliye mdogo hadi mkubwa zaidi ya wote, mfalme na wote, hakuchezea mtu ye yote. Bali iliwabidi kujua alikuwa nabii. Hawakuweza kujuziua kujua jambo hilo. Ndiyo, bwana.

¹⁰⁶ Hata Ahabu alijaribu kumshitaki kwa ajili ya ukame. Naye kweli alimwomba Mungu apeleke ukame. Ndiyo, aliomba. Naye akasema, “Nina mamlaka na nitafunga mbingu; hata haitanyesha, au umande hautaanguka, hata nitakapouagiza.”

¹⁰⁷ Ungeweza kuwazia maskini Yezebeli akiwa na huo uso uliopo dolewa, akikanyaga kwa nguvu huku na huko sakafuni, “Maskini mnafiki huyo! Maskini mnafiki huyo, akiwafanya watoto hawa wote wadogo kupata taabu,” na yote hayo. Eliya alikuwa anajaribu kuwarudisha kwa Mungu, akijaribu kulirudisha taifa kwa Mungu. Unaona? Na inaonekana kama angeweza kuwaambia hao watu, “Na unataka kuniambia ungemwamini mtu kama huyo, ambaye angefunga nchi hivi, na wala isinyeshe mvua au umande? Na unafiki wake wote au uchawi wake nje huko,” lo lote alilotaka kuliita. “Naye si kitu ila tu m—mchawi au mnajimu, au kitu fulani. Amefunga mbingu na haitanyesha, akiwafanya watu hawa wote wateseke. Na basi unasema hayo ni mapenzi ya Mungu?”

¹⁰⁸ Yalikuwa ni mapenzi ya Mungu! Haidhuru nini, unaona, yakubidi uangalie nini. . . Yakubidi umheshimu Mungu bila ya kujali nini Yeye anatenda. Yeye anajua analofanya. Lilionekana jambo baya watoto wakiteseka, watu wakiteseka, ng’ombe wakifa, kondoo wakifa, hakuna maji po pote, usiku ulikuwa na joto na wenye jasho jua lilikuwa linawaka kama shaba mbinguni mchana, kwa miaka mitatu na miezi sita. Naye Eliya akiketi mlimani, akasema, “Hakutakuwa na umande wala mvua ila kwa neno langu.” Hilo ni kweli. Loo, jinsi walivyomchukia!

¹⁰⁹ Na wakati yeye, Ahabu alipomwona, akasema, “Wewe ndiwe unayeitaabisha Israeli, sivyo?”

¹¹⁰ Mzee Eliya akatazama nyuma usoni mwake, akasema, “Hasha, si mimi, bali ni wewe unayeitaabisha Israeli.” Hiyo ni kweli. Unaona, hata Ahabu hakumheshimu. Na unajua ambalo Eliya alimwambia Ahabu, kasema, “Kwa sababu umemwaga damu isiyi na hatia ya Nabothi, vivyo hivyo mbwa watairamba damu yako, pia, barabarani.” Nao waliiramba! Kwa sababu hawakumheshimu mjumbe wa Mungu. Hiyo ni kweli kabisa. Hawakuiheshimu.

Sasa, Miriamu hakuiheshimu. Haruni hakuiheshimu.

¹¹¹ Haidhuru wewe u nani, Mkristo au si Mkristo, bado yakubidi kuleta heshima kwa Mungu, na uheshimu anachofanya, la sivyo utajuta. Ni aidha kulipokea ama kwenda hukumuni, mojawapo unalotaka.

¹¹² Jinsi ningeweza kusimama na ushuhuda, saa baada ya saa, wa yale nimeona katika maisha yangu, ambayo nimeona katika nchi zingine na sehemu nyingine za mataifa, na kadhalika, mambo ambayo yametukia. Lakini tuliache hilo, ili kwamba tu upate wa—wazo la ambalo ninajaribu kukuambia, lazima uiheshimu. Nimeona vijana wakiketi katika mkutano, na

kujichekea na kucheka mkutanoni, na, haijapita masaa ishirini na manne, wanapondwapondwa barabarani. Nimewaona vijana wakiketi katika mkutano, mnamo mwaka mmoja nilipokuwepo mahali, halafu, labda mnamo miezi sita, nikarudi sehemu ile ile, na karibu kila mmoja wao ameaga dunia, au ameuwawa, ameugua mahali fulani, kwa maradhi na kadhalika. Hilo ni kweli. Yakubidi uiheshimu.

¹¹³ Ninamkumbuka msichana mmoja usiku mmoja, huko Tennessee, nilipokuwa mlangoni ninatoka nje, nilipohubiri katika kanisa kubwa la Kibatisti, nilikuwa mlangoni nikitoka. Nami nilijisikia kuongozwa usiku ule kumwita aje kwa Kristo. Naam, alinicheka usoni mwangu nilipomwita amjie Kristo. Ikawa kwamba yeye alikuwa mmoja wa binti za shemasi. Basi huku amesimama mlangoni usiku ule, aliningojea. Basi nikatoka, akasema, “Nakutaka ujue kitu fulani sasa hivi, usinitahayarishe namna hiyo tena.”

Nikasema, “Mungu alikuwa anakuita.”

¹¹⁴ Akasema, “Upuzi! Mimi ni kijana,” akasema, “ninao muda mwingi kwa jambo hilo.” Kasema, “Baba yangu anayo dini ya kutosha kwa ajili yetu sote nyumbani.”

¹¹⁵ Nikasema, “Haikutoshi wewe, dada, kila mmoja yambidi awe na dini yake mwenyewe.”

¹¹⁶ Akasema, “Kama nikitaka mtu ye yote anizungumzie kuhusu jambo hilo, nitampata mtu mwenye akili, si mtu kama wewe.”

¹¹⁷ Nikasema, “Nenda, sema unalotaka kusema, huniudhi, ila siku fulani utalijutia.”

¹¹⁸ Si muda mrefu baada ya hayo, nilipita kwenye mji ule ule. Huyu hapa anakuja barabarani na kirinda chake cha ndani kikining’inia nje, huku akiyumbayumba na sigara mkononi mwake, naye akanikaribisha wiske. Jambo lile lile! Na huu ndio ushuhuda wake, alisema, “Unakumbuka usiku ule ulioniita pale?” Kasema, “Ile ilikuwa ni kweli.” Akasema, “Roho wa Mungu alikuwa akinishuhudia usiku ule, akijaribu kunivuta nje.” Naye akasema, “Tangu hapo niliweza kuona nafsi ya mama yangu ikikaangwa kuzimu kama andazi, na kuicheka.” Hilo ndilo lililotendeka, unaona.

¹¹⁹ Yakubidi kumheshimu Mungu. Ni hilo tu. Yakubidi kulitenda hilo, ndugu. Ni hilo tu. Yezebeli hakuiheshimu.

¹²⁰ Pia kumbuka wakati mwingine, kulikuwa na baadhi ya watoto wasiokuwa na adabu, walilelewa kwenye nyumba fulani.

¹²¹ Eliya, baada ya siku zake, bila shaka, watu walimchukia kwa sababu aliagizia ile njaa nchini. Kulikuwa na baadhi ya watu ambao waliwafundisha watoto wao kwamba “Eliya, mtu kama huyo,” ameshabadilishwa na kuchukuliwa Mbinguni.

“Ameuwawa mahali fulani, nao walimzika tu na kumficha.” Wao—wao hawakuliadini.

¹²² Kwa hiyo Elisha alichukua mahali pake, sasa yeye alikuwa mjumbe wa siku ile baada ya Eliya kutwaliwa. Kwa hiyo alipita kwenye mji fulani, na hao watoto, watoto wadogo wa mji ule, wakatoka mbio, wakimdhaki, kasema, “Aisee, mzee kipara wee, kwa nini hukunyakuliwa kama Eliya?” Unaona, hawakuamini Eliya alitwaliwa. Ndivyo ilivyo. Haikuwa kutomheshimu mtu yule; ilikuwa kutomheshimu Ujumbe wake. Alikuwa halifa wa Elisha, wa Eliya. Alikuwa na upako, roho wa Eliya alikuwa juu yake. Alikwenda moja kwa moja kule akafanya mambo yale yale ambayo Eliya aliyafanya. Haleluya!

¹²³ Yesu alisema, “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi yeye naye atafanya.” Ndiyo. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

¹²⁴ Hawakuliheshimu. Na hawakumheshimu Eliya kwa sababu alimwamini Elisha, kwa sababu Roho alikuwa juu yake. Naye akageuka akaupiga Yordani kwa vazi lake, na akaufungua Yordani, akaondoka akaenda akafanya miujiza ile ile ambayo Eliya alifanya. Na hata wahubiri wote pale kwenye shule ya manabii, wakasema, “Roho ya Eliya inakaa juu ya Elisha,” ikaenea nchini.

¹²⁵ Na watu, nina hakika walicheka mmoja kwa mwenzake, kasema, “Ha-ha, ha-ha, tazama, tazama kule. Lile kundi la watakatifu wanaojifingirisha, shupavu wa dini, wakisema, ‘Mtu yule alikwenda Mbinguni bila kufa, farasi walishuka chini.’ Hatukuona hata mmoja.” Hakika hawakuwaona. Hasha, hawakuwaona. “Hatukuwaona farasi wo wote. Hatukusikia magari yo yote po pote. Upuzi! Mzee yule alikufa nao wakamzika, na halafu wanajaribu maigizo mengi.”

Ni kama tu vile wangelisema leo, jambo lile lile!

¹²⁶ Kama walivyosema kumhusu Yesu, walisema, “Mbona, walikuja wakauiba mwili Wake usiku.” Hata waliwahonga askari kushuhudia hayo. Lakini Yeye alifufuka katika wafu!

¹²⁷ Na Eliya alitwaliwa juu katika gari la moto, na farasi wa moto.

¹²⁸ Na nabii huyu kijana alipotembea pale, akipita mjini. Naye alikuwa amenyonyoka nywele zake, akiwa kijana mwanamume. Alikuwa anashuka, kwa hiyo hawa watoto wadogo wakakimbia nyuma yake, kasema, “Wee, kwa nini hukuwenda juu pamoja na Eliya?” Kasema, “Ewe mzee kipara, wewe!” Unaona? Nao walikuwa hawampi heshima. Basi Eliya alifanya nini? Aligeuka, katika nguvu za Roho, akawalaani hao watoto. Nini kilitukia? Dubu jike wawili walitoka mwituni wakawaua arobaini na wawili kati yao. Sawa. Kukosa heshima, kutokuwa na kicho. Huwezi kufanya hivyo. Yakubidi umheshimu Mungu.

¹²⁹ Kama ye yote wa hao watoto angesema sasa, kama baba yao na mama wangesema, “Sasa, angalieni, enyi watoto, wanasema kwamba Eliya alitwaliwa juu. Sasa, hatujui kuhusu hayo, lakini, kwa vyo vyote, si—si—sijui kama ndivyo ilivyo au sivyo, lakini nawaambia kitu bora sana cha kufanya ni kutosema cho chote juu yake. Endeleeni tu. Atakapopita... Tunasikia anashuka kuja apite mjini leo, atakuwa na mkutano wa mitaani juu kule. Akifanya hivyo, ninyi watoto mnapokwenda shuleni leo, mkikutana naye, hebu semeni tu, ‘U hali gani, kasisi? U hali gani, bwana?’ Au jambo kama hilo. Zungumzeni naye.”

¹³⁰ Lakini badala yake, bila shaka walikwisha ambiwa huko nyumbani, loo, waliwasikia baba na mama wameketi mezani wakicheka, mmoja kwa mwingine, wakisema, “Una habari! Walisema yule maskini mtakatifu anayejifingirisha alitwaliwa juu. Mlipata kuamini jambo kama hilo? Nao wakasema huyu mzee upara, kipara kama boga kule, hana zaidi ya miaka thelathini na mitano, na hapa anashuka akipitia pale, nao watakuwa na mkutano wa mitaani, wanafikiri sisi tutaamini upuzi kama huo. Mbona, yeye si kitu ila maskini mwi—mwigizaji tu. Ni hivyo tu. Maana, yeye hatakuja kanisani mwetu yeye ni kama tu Eliya alivyokuwa, hatakuja kanisani mwetu. Sisi, ata... Labda aina fulani ya uchawi, voodoo, mazingaombwe aliyo nayo, kama Eliya.” Hawakumwamini. Kwa hiyo, watoto walifundishwa hayo huko nyumbani.

¹³¹ Kama wangelifundishwa kicho na heshima, wangelikwenda pale mbele ya nabii yule wa Mungu na kumtaka awaombe dua.

¹³² Lakini walikuwa wamefundishwa kujichekea na kucheka, na kudhihaki. Ni kama watoto wa siku hizi, la, wengi wao leo watadhihaki mkutano wa mitaani, watadhihaki kuhubiriwa kwa Injili.

¹³³ Kwa hiyo, Eliya aliwalaani, katika Jina la Bwana. Si kwa sababu ya watoto, lakini kwa sababu ya wazazi wasio na kicho ambao wamewalea watoto namna hiyo kutokumheshimu Mungu. Dubu wawili wa kike wakatokea na kuua arobaini na wawili wao. Sasa, huko ni kutokuwa na kicho. Mungu hudai heshima! Walipokosa kumheshimu nabii Wake, wao walimvunjia Yeye heshima, haidhuru kama hawakuamini, iliwabidi kufunga midomo yao, wajitenge na jambo hilo. Lakini, wapi, iliwabidi kuonyesha ustahiki wao. Iliwabidi kusema jambo fulani ambalo halikuwapasa kusema. Basi nini kiliwapata?

¹³⁴ Hebu tuchukue baadhi ya watu ambao waliiheshimu. Hebu tumchukue yule mwanamke Mshunami, kwa nabii yule yule, Eliya. Kwa kweli hakuwa Mwisraeli. Alikuwa anatoka Shunemu, lakini alimwamini Mungu. Naye alimwona mtu huyu akipita mjini, akamsikia akizungumza, aliona ishara ambazo alitenda.

¹³⁵ Imesimuliwa katika historia, sijui kama ni kweli au la, kwamba siku moja kundi la mbwa mwitu lilikuwa likijaribu kumkamata msichana mdogo. Naam, hili si Maandiko, ni hadithi tu niliyoisoma. Na ilisema yule mwanamke Mshunami alikuwa amesimama pembeni, naye aliona kwamba mbwa hawa watamuua msichana huyu mdogo. Naye mtu huyu mtakatifu alikuwa anapita mjini, naye akainua fimbo yake kwa Mungu, naye akawaombea rehema hao watoto wadogo namna hiyo, kisha hao mbwa wakageuka wakawaacha. Kama ni kweli au la, inaonekana kama ingeweza kuwa kweli, sijui.

¹³⁶ Lakini, kwa vyo vyote, mwanamke huyu alisema, wakati Biblia, wakati yeye “alitambua kwamba huyu alikuwa mtu mtakatifu.” Alitambua jambo fulani limetukia. Aliona yeye alikuwa nani, na “akatambua kwamba yeye alikuwa mtu mtakatifu aliyetoka kwa Mungu.” Na, badala ya kutokumheshimu kama Yezebeli alivyotenda, alimheshimu. Akamwambia mumewe, “Sisi tunaweza kabisa kutenda jambo hili. Nakuomba, tumjengee nyumba ndogo nje hapa mahali fulani. Hebu na tumpe mahali padogo, kwa maana amechoka. Nimemwangalia. Anazeeka, na ninaona nywele zake zenye mvi zikining’inia chini katika ndevu zake. Fimbo yake ndogo kuukuu, mikono yake midogo iliyokonda anapotembea, mikono midogo dhaifu namna hiyo. Na huyu hapa yuaja akitembea, amebeba chupa ndogo ya mafuta ubavuni mwake, na kipande cha ngozi ya kondoo kimefungwa mwilini mwake, kwenye jua kali, mwili wake ulionekana umechomwa na ni mwekundu. Nami ninakuomba, hebu na tumtengenezee kituo kidogo, akapumzike hapa. Hebu tumtafute mjezi aje hapa amtengenezee kijumba kidogo, akaishi humo, kwa sababu ninatambua kwamba roho yake, kwa roho yake, yeye ni mtu mtakatifu. Ni mtu wa Mungu.” Loo, loo, ni tofauti jinsi gani!

¹³⁷ Sasa, mumewe alikubali, yeye...mwanamume huyu pengine angelisema, “Mpenzi, mimi nimemwangalia mtu huyo, pia. Nimemsikiliza, nimemwangalia, nimeona kazi zake. Najua ni mtu mtakatifu wa Mungu. Kwa hiyo tutafanya tu jambo hilo.” Kwa hiyo walimwita mjenzi naye akamjengea nyumba ndogo nzuri, na wakamwekea kitanda kidogo pale cha kupumzikia kusudi apate kulala na kupumzika. Wakamtengenezea mahali pa kuoshea miguu yake, wakachukua maji na kadhalika, wakayaweka pale.

¹³⁸ Basi yule nabii alipokuja, bila shaka, hilo lilibariki nafsi yake kuona kwamba jambo fulani lilikwisha tendeka kwa ajili yake. Akamwambia Gehazi, “Nenda, ukamwite, ukamuulize kitu gani ningeweza kumtendea, ningeweza ‘kuzungumza na mfalme, na kapteni mkuu?” Yeye. . .

¹³⁹ Mwanamke akasema, “Ninaishi miongoni mwa watu wangu, na hakuna kitu ninachohitaji.”

140 Lakini Gehazi akasema, “Hana watoto. Na mumewe amekuwa mzee sana, ni mzee. Hawana watoto.”

141 Halafu ningewazia, Eliya akikaa pale kwenye kitanda hiki kidogo ambacho amembariki yeye kwa kukitengeneza, alinawa miguu yake, na ndevu zake zimesafishwa zote, na mambo yote, akilala pale, bila shaka aliona ono la Bwana (sababu sikuzote walitenda jambo hilo). Kwa hiyo alisema, “Nenda, kamwite, ukamwambie asimame hapa mbele zangu.” Loo, jamani! “Nenda ukamwite, kwa sababu yeye ame—amemheshimu Mungu. Nenda, kamwambie aje hapa.”

142 Aliposimama mlangoni, akasema, “BWANA ASEMA HIVI. Mnamo wakati kama huu mwakani, utamzaa mtoto.” Na mnamo wakati kama ule mwakani, akapata mtoto.

143 Halafu Shetani, alipopata kuwa na umri wa miaka kumi na miwili, babaye alimpeleka shambani siku moja, ndipo Shetani akasema, “Nitamwangamiza mtoto yule,” kwa hiyo akamwambukiza homa ya jua. Naye akafa katika mikono ya mamaye.

144 Je! hilo lilimvunja moyo? La, bwana. Alisema, “Tandika nyumbu. Kisha utangulie, usisimame. Nenda hadi mlima Karmeli, mlimani, kwa sababu yeye amepita hapa juzijuzi.” Loo, loo, loo jamani! Ndivyo ilivyo. Basi ndizo heshima. Hizo ndizo heshima.

145 Ndipo mumewe akasema, “Unakwenda kwa yule mtu wa Mungu.” Akasema, “Wala si mwezi mchanga au sabato, hatakuwa juu kule katika ninino yake. . .”

146 Akasema, “Kila kitu kitakuwa salama, hebu mtandike nyumbu uniache niendele.” Hivyo basi wakaenda zao.

147 Nao wakapanda mlimani. Na wakati mzee Eliya alipotazama nje ya pango, kisha akatoka pale akaangalia nje, naye kasema, “Huyu anayekuja anaonekana kama yule mwanamke Mshunami.” Kasema, “Hapana budi ana huzuni.” Akasema, “Nenda, kamlaki. Na, ingawaje,” kasema, “ana huzuni moyoni, na Mungu hakuniambia neno juu yake.”

148 Unaona, si lazima Mungu akuambie kila kitu, unaona, kwa hiyo hata hawaambii manabii Wake kila kitu. Huwa tu—Yeye hutenda tu analotaka kutenda, Yeye ni Mungu.

149 Hapa, sasa, Eliya akasema, “Mungu!” Vipi kama Eliya angesema hivi, “Mbona Wewe hukuniambia kwa nini anakuja? Mbona Wewe hukuniambia hayo yote?” Asingaliona kamwe kitu. Lakini ilikuwa sawa kwa Eliya, haidhuru.

150 Basi vipi kama angalikuja na kusema, aseme, “Ulisema ulikuwa mtumishi wa Mungu? Mnafiki wee! Ninaamini wewe si kitu ila mtakatifu anayejifingirisha”? Lisingetukia. Unaona? Mungu hutujaribu wakati mwingine, aone tutakalotenda.

¹⁵¹ Kwa hiyo, badala ya jambo hilo, alimkimbilia miguuni pake akasujudu, kama anayemsujudu Mungu. Naye akasema, naye akamfunulia kuna nini. Naye Eliya akasema, “Chukua fimbo yangu uende ukaiweke juu ya huyo mtoto.”

¹⁵² Naye alipoitwaa, yule mwanamke akasema, “Kama aishivyo Bwana Mungu, na nafsi Yake isivyokufa,” loo, jamani, “ewe mtu wa Mungu, sitakuacha. Nitaketi hapa mpaka Mungu atume ono.” Mzee Eliya akakaa pale kwa muda kidogo zaidi; akajifunga mshipi kiunoni mwake, akaitwaa fimbo yake akaenda zake.

¹⁵³ Akaingia chumbani ambapo yule mtoto alikuwa amelala, mtoto aliyekufa. Akatembea huku na huko sakafuni, namna hiyo, mara chache. Kwa sababu ya mwanamke mwenye kicho, mwanamke ambaye alimheshimu, mwanamume ambaye alimheshimu, na kuamini kwamba yeye ni mtu wa Mungu, alienda mbele akarudi nyuma na kutembea huku na huko sakafuni mpaka Mungu akamjibu. Amina. Halafu akajilaza mwenyewe juu ya mtoto yule naye akapiga chafya mara saba, akamchukua akampa mamaye. Akaondoka akaenda zake, naye akarudi pangoni. Kwa sababu alimheshimu yule mtu wa Mungu! Amina. Mungu anadai heshima.

¹⁵⁴ Na Martha je? Alikuwa sikuzote anafikiria juu ya kumtengenezea Yesu mlo mtamu. Mariamu alitaka kusikiliza Neno la Mungu, kwa hiyo aliketi tu hapo akamsikiliza Yeye. Hakujali kama foronya zilibadilishwa, au kama yale—mapazia yalikung’utwa vumbi, au kama walikuwa na chakula au la, yeye alitaka tu kusikia ambayo Yesu alitaka kusema. Lakini Martha sikuzote alitaka kumpikia Yeye mlo mtamu, na kuhakikisha kwamba kiti kimewekwa mito vizuri na kimewekwa sawasawa tu, na kila kitu kimesafishwa namna hiyo. Lakini alimtaka Yeye, kumfanyia Yesu jambo fulani katika njia yake, na Mariamu alitaka kulitenda katika njia yake. Lakini siku moja wakati Lazaro alipokuja . . . Watu wengine huzungumza dhidi ya Martha, wanasema, ingelimpasa kuwa makini zaidi. Loo, hashu, hebu kidogo. Unaona, ulifika wakati wa Martha kuonyesha yake. Ndipo basi wakati Yesu . . . Wakati Lazaro alipokufa, ndugu yake, alimwomba Yeye aje akamwombe. Yeye hakuja. Alipuuza huo mwito, akaenda kwingine. Akatuma tena, Yeye akazidi kuupuuza huo mwito.

¹⁵⁵ Bali hatimaye Yeye alipokuja, ilionekana kama sasa angeweza kumwendea Yeye na kusema, “Kwa nini Wewe hukuja? Sababu gani Wewe hukuja nilipokuja? Kaka yangu alikuwa amelala pale, mgonjwa. Tumeacha kanisa letu, tumeacha madhehebu yetu, tumefanya kila kitu kuufuata Ujumbe Wako, kwa maana tuliamini ya kwamba Wewe ni mtu wa Mungu. Lakini Mtu wa Mungu angewezaje . . . Na sisi wawili ni yatima, watoto watatu yatima, watu watatu yatima, na kazi yetu ilikuwa ni kutengeneza mazulia ya hekalu. Tulikuwa washiriki kule, mama yetu na baba yetu walikuwa washiriki kule. Lakini kwa

sababu ulitudanganya tukaingilia jambo fulani, kuamini mambo haya ambayo Wewe unajaribu kufundisha, ukisema kwamba Wewe ni Mwana wa Mungu na Nabii aliyetumwa kutoka kwa Mungu, na mambo haya, tutawezaje kukuamini Wewe, Mtu ambaye hata hatanisikia ninapokuita Wewe? Nilipokuwa katika haja na nikakuhitaji, Wewe uliupuuza ujumbe wangu ukaenda Zako. Kisha nikatuma tena, ukazidi kupuuza. Mbona ukatenda jambo kama hilo?” Kama angalifanya hivyo, hadithi hiyo ingekuwa tofauti usiku wa leo.

¹⁵⁶ Alifanya nini? Alimkimbilia moja kwa moja mahali Yeye alipokuwa, akaanguka chini miguuni Mwake akasema, “Bwana, kama Wewe ungalikuwepo hapa, ndugu yangu hangalikufa.” Loo, ndivyo ilivyo. Alikuwa anafanya nini? Alikuwa anaheshimu. Alikuwa katika Uwepo wa Mungu, naye akamheshimu Yeye. Alimwita Yeye Bwana wake. “Bwana, kama ungalikuwa hapa.” (Si, “Nilituma ukaitwe!” Hayo yote yalisahauliwa.) “Sasa uko hapa, unaona. Kama ungalikuwa hapa, ndugu yangu asingalikufa.”

Yeye akasema, “Ndugu Yako atafufuka tena.”

¹⁵⁷ “Loo,” akasema, “ndiyo, Bwana, najua atafufuka tena siku ya mwisho.”

¹⁵⁸ Na—Naye akasema, yeye... Yeye akasema, “Lakini Mimi Ndiye Ufufuo na Uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ingawa amekufa, bali ataishi. Kila aishiye na kuniamini Mimi, hatakufa kabisa hata milele.”

¹⁵⁹ “Naamini, Bwana, kwamba Wewe u Mwana wa Mungu ajaye ulimwenguni. Na hata sasa, Bwana!” Loo! “Hata sasa!” (Sio, “Bwana, ilikupasa Wewe kufanya *hili* na ilikupasa kufanya *vile!*”) Bali, “Hata sasa, lo lote Wewe utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa.” Naam.

¹⁶⁰ Vipi kama tungeliweza kusema hayo kwa mtu fulani usiku wa leo, “Loo, ndugu yangu, ninaamini kwamba utakachomwomba Mungu, Mungu atakupa wewe?” Matokeo yale yale yangetokea.

¹⁶¹ Lakini haidhuru Yeye alikuwa hivyo kiasi gani, kama Yeye alikuwa... Nasi tunajua Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Kama angalilidharau, lisingetendeka kamwe. Hayo yalitokea moyoni mwake. Akasema, “Hata sasa, Bwana, lo lote Wewe utakalomwomba Mungu, Mungu atakupa Wewe.” Ndivyo ilivyo. Ndivyo ilivyo. Toka moyoni mwake, yeye aliliamini. Kama Yeye angefanya safari ya kuwinda au safari ya uvuvi, hilo ni mamoja kwake.

¹⁶² La, kama Eliya angalifanya safari ya kuwinda au angekwenda mahali fulani, kwake ni mamoja, kwa yule mwanamke Mshunami. Bado yeye alimwamini kuwa mtu wa Mungu. Hakika. Haidhuru yeye alitenda nini, bado alikuwa mtu

wa Mungu, kwake, kwa sababu amemwona Mungu akitenda kazi maishani mwake.

¹⁶³ Na, kwa Martha, haidhuru jambo gani lilitukia, amekwishaona ambalo Mungu amemtendea yeye. Akasema, “Hata sasa, Bwana, lo lote Wewe umwombalo Mungu, Mungu atakupa Wewe.” A-ha, ni hivyo basi.

¹⁶⁴ Akasema, “Ndugu yako atafufuka tena.” Na kwa hiyo Yeye akasema, “Mumemzika wapi?” Nao wakashuka kwenda kaburini. Naye akamwita Lazaro toka kaburini, baada ya kufa siku nne. Kwa nini? Kwa maana dada ya Lazaro aliheshimu kile Yeye alichokuwa.

¹⁶⁵ Kama huwezi kumheshimu huyo mtu, iheshimu kazi anayomfanyia Mungu. Hilo ni sawa kabisa, unaona, mheshimu. Kama mchungaji akija, mchungaji wako, sikuzote mheshimu. Nimesikia makusanyiko yakizungumza juu ya mchungaji wao, kila kitu juu yake, wakimsengenya, kumdhihaki. Mchungaji huyo atawezaje kukutendea jambo lo lote? Hawezi kulitenda. Wewe—wewe huwezi, wewe huwezi ku. . . Sineni juu ya kanisa hili, bali ninamaanisha makanisa niliyoona, ya kwamba kama wewe. . . Unapaswa kumpenda mchungaji wako. Yakubidi kujua kwamba yeye ni mwanadamu, lakini hata hivyo Mungu amemfanya kuwa mchungaji Wake. Roho Mtakatifu amemfanya yeye mwanagalizi, basi yakubidi kumheshimu yeye kwa jinsi hiyo. Na haidhuru mchungaji amefanya nini, kama ukimheshimu yeye moyoni mwako, kama mtumishi wa Mungu, Mungu atakuheshimu kwa kutenda jambo hilo.

¹⁶⁶ “Yeye ambaye—yeye anipokeaye Mimi, anampokea Yeye aliyenipeleka,” Yesu alisema. “Yeye ambaye hanipokei Mimi, hawezi kumpokea Yeye.” Unaona, walisema Mungu alikuwa Baba yao; Yeye alisema, “Baba yenu ni Ibilisi.”

¹⁶⁷ Kwa hiyo, unaona, yakubidi kuliheshimu hilo na kuliamini, amini kwamba Yeye ndiye. Ndiyo, Martha aliliamini.

¹⁶⁸ Na hilo ni jambo moja dogo nililogusia asubuhi hii, wakati alipokuja yule mwanamke Msirofoinike. Tazama jinsi alivyokataliwa, kwa uchungu. Huyo hapo, alikuwa Muya hudi; na mwanamke Mtaifa, naye alimewendea Yeye mbio. Hakujua jinsi ya kumwendea Yeye, lakini alikuwa na haja, naye alijua kwamba huyo alikuwa Mwana wa Mungu. Aliamini. Yeye. . . Kama—kama Mungu angejibu sala Yake kwa ajili ya wengine, Yeye angejibu sala kwa ajili yake. Naye alijua alilosema Yeye ni Neno la Mungu. Kama lilikuwa Neno la Mungu kwa Wayahudi, lilikuwa Neno la Mungu kwa Mataifa, pia, lo lote alilosema Yeye. Naye Yesu akampa jaribio. Alisema, “Bwana, nirehemu!” Sasa tazama. La, kasema, “Ewe Mwana wa Daudi,” sababu amesikia Wayahudi wakisema, “Ewe Mwana wa Daudi.” Sasa, Yeye hakuwa Mwana wa Daudi kwake. Unaona? Akasema. . . “Ewe Mwana wa Daudi!” Hivyo ndivyo Myahudi

angeliliendea, sababu aliwasikia wengine wao. Alijaribu kuja kama walivyofanya, sababu alikuwa akijaribu kupata heshima. Alikuwa akijaribu kutoa heshima zake. Naye hakuwa tu akijifanya; Yesu angejua kama ilikuwa kujifanya. La, Yeye angelijua. Kwa hiyo alipokuja, alisema. “Ewe Mwana wa Daudi, mrehemu binti yangu, kwa sababu amepagawa sana na pepo.”

¹⁶⁹ Yeye aligeuka akamwanguka, akasema, “Si vema Kwangu kukichukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa.” Whiu! Si ni jambo kwelikweli? Hilo ni jambo kwelikweli! Si kwamba tu alimkatalia ombi lake, bali alimwita yeye “mbwa.” Hilo ni kweli. Na mbwa ni moja ya majina mabaya sana iliyo nayo Biblia, unajua. Kwa hiyo Yeye alisema, “Si vema Kwangu kuchukua chakula cha watoto na kukitupia mbwa.”

¹⁷⁰ Akasema, “Hiyo ni kweli, Bwana.” “Bwana,” hapo akalipata. Yeye hakuwa Mwana wa Daudi kwake, bali Yeye alikuwa Bwana. Kasema, “Kweli, Bwana. Hiyo ni kweli, lakini watoto hula makombo chini ya... Au, ninamaanisha, m—mbwa hula makombo chini ya meza ya bwana.” Naam. Basi. Hiyo ilikuwa heshima.

¹⁷¹ Yesu alimgeukia, akasema, “Imani yako ni kubwa. Sasa nenda nyumbani, utamkuta binti yako kama tu ulivyoamini.” Basi. Kwa nini? Ilikuwa ni jinsi alivyoliendea.

¹⁷² Vipi kama angegeuka na kusema... Yeye aligeuka, kasema, “Si vema Kwangu kuchukua...” Kwa maneno mengine, “Si sawa.”

¹⁷³ Tuseme, Mkatoliki anakuja na kusema, “Ee, Ndugu Branham, ninajua Mungu huyasikia maombi yako kwa ajili ya watu hawa hapa. Utaniombea?”

¹⁷⁴ Nami ningesema, “Vema, si vema kwangu mimi kupoteza wakati wa watoto hawa hapa. Nipo hapa kuwaombea hawa Wapentekoste, sio ninyi kundi la Wakatoliki.” Unaona? Je! angesema nini? Loo, jamani, nawazia angetoka hapa kwa hasira sijui kama nini. Unaona?

¹⁷⁵ Lakini aligeuka akasema, “Hilo ni kweli, Bwana. Hilo ni kweli, Bwana. Lakini tuna—tunakubali hivyo, mbwa wanakubali kula makombo chini ya meza ya Bwana.”

¹⁷⁶ Unaona, hilo lilimpata Yeye haraka sana. Yeye aligeuka akasema, “Imani yako ni kubwa.” Na halafu tunaona tukio jingine... Unaona, ilikuwa jinsi alivyoliendea, heshima zake. Alikuwa anamheshimu Mungu alipomheshimu Yeye.

¹⁷⁷ Kwa hiyo tunaona wakati mmoja kulikuwa na Mrumi, naye alikuwa mtu mashuhuri, pia aliwapenda Wayahudi. Naye alikuwa na mtumishi mgonjwa. Yeye mwenyewe, hakujisikia anastahili kwenda kumwomba Yesu.

¹⁷⁸ Unaona, sikuzote unataka kujisikia mdogo zaidi kuliko ulivyo. Usiwe mkubwa mbele ya macho yako mwenyewe.

Unaona? Sasa, na kama u mkubwa, acha mtu mwingine aseme hivyo juu yako. Unaona? Lakini sasa wakati wewe, mwanamke huyu au. . .

¹⁷⁹ Mtu huyu, hasa, alisema alikuwa akida wa Kirumi naye alikuwa na mtumishi mgonjwa, kwa hiyo alituma ili huyu mtumishi mgonjwa aponywe. Naye Yesu akasema, “Nitakuja nipate kumponya.”

¹⁸⁰ Kwa hiyo Yeye alipokuwa anaenda, yule Mrumi alimwona akija. Nafikiri alisema, “Loo, jamani, hapa yuaja Yule Mtakatifu. Hapa yuaja Yule Mtakatifu. Naam, mimi ni Mtaifa bure. Mimi—mimi—mimi ni akida wa Urumi. Mimi ni Jenerali, au—au afisa. Mimi—mimi—mimi kwa kweli si Myahudi, sina haki kwa Yule Mtu Mtakatifu kuja.” Unaona heshima? Unaona? “Sina haki kwa Yule Mtumishi Mtakatifu wa Mungu kuja nyumbani kwangu.”

¹⁸¹ Alimwona anakuja mlangoni, akamwita, kasema, “Bwana, mimi—mimi sistahili kwamba Wewe uingie chini ya dari yangu.” Labda alikuwa na jumba la fahari, yule akida. Kasema, “Sistahili kwamba Wewe uje chini ya dari yangu. Nami—mimi sikujifikiria mwenyewe kuwa hata nastahili kuja Kwako, kwa hiyo nilituma baadhi ya watu Wako—Wako Mwenyewe waliobarikiwa, hao Wayahudi. Lakini nina mtumishi hapa ambaye ni mgonjwa sana.” Naye akasema, “Mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka,” kasema, “nikimwambia askari huyu, ‘Nenda,’ huenda. Namwambia huyu, ‘Njoo,’ anakuja.”

¹⁸² Alisema nini hapo? “Ninajua kwamba Wewe una mamlaka yote. Wewe unaweza kuuambia ugonjwa huu, ‘Nenda,’ na uende. Na unaweza kuuambia huu, ‘Njoo,’ nao ungekuja.” Unaona, Yeye alitambua. Na kama vile yeye alivyokuwa na mamlaka juu ya askari hawa, vivyo hivyo Yesu alikuwa na mamlaka juu ya maradhi yote na magonjwa. “Jambo pekee likupasalo kufanya, Bwana, ni kusema Neno tu! Hivyo tu! Sema Neno tu, mtumishi wangu ataishi.”

Yesu akasimama, akawageukia Wayahudi, akasema, “Sijaona imani kama hivyo katika Israeli.”

¹⁸³ Akasema, “Ni vema kwa mtumishi wako.” Amina. Kwa nini? Kwa maana yeye aliliheshimu. Alimheshimu Yesu Kristo Ambaye alikuwa Mu—Mungu wa Mbinguni.

¹⁸⁴ Sasa, nadhani wakati unaenda sana, nataka tu kusema jambo moja zaidi, ndilo hili. Heshima hizo zote kubwa, na kadhalika; lakini leo, kwa namna fulani, ni tofauti. Mungu anaweza kutenda jambo fulani leo, na watu watalicheka. Naamini kwamba tungepaswa kuwa tofauti leo, yapata miaka arobaini iliyopita wakati Roho Mtakatifu alipoanza kushuka kwa mara ya kwanza, lakini watu walifanya nini? Waliwafunga wahubiri, wakawaita watakatifu wanaojifingirisha. Walitoka wakaenda kwenye. . . Hata hawangaliwalisha chakula mijini, na

kila kitu namna hiyo; nao walivunja mahindi kwenye njia za reli, wapate kuishi. Walifanya nini? Walikuwa na miaka mingine arobaini, kanisa linayo, likiteseka, limepitia kila kitu, vita viwili mnamo muda kama huo, unaona, imewaua maelfu yao; ambapo, lingekuwa labda limekwisha kwenda Nyumbani.

¹⁸⁵ Sasa, kungetukia nini, wakati Mungu ameanza kumwaga Roho Mtakatifu juu ya kanisa katika siku za mwisho, kungetukia nini miaka ishirini na mitano iliyopita wakati Yeye alipoanza kushusha ishara Zake na maajabu na miujiza, nini kingetukia kama watu wangeliumkana pamoja? Walifanya nini? Walisema “Ni voodoo, ni kiinimacho, yeye ni mjanja wa kushirikishana mawazo, yeye ni *hili, lile, au jingine*.” Vipi kama mataifa yote yangelikwenda pamoja na kusema, “Jina la Bwana libarikiwe”? Vipi kama Wamethodisti na Wabatisti, na Wapresbeteri na hao wote, wangeungana pamoja na kusema, “Asante Mungu, haya ndiyo tumekuwa tukiyatazamia. Roho Mtakatifu anamwagwa. Mbona, hawa hapa watu wanaoona maono, hawa hapa manabii miongoni mwetu, hivi hapa—hivi hapa vipawa vile vipawa vyote vikuu, wananaji kwa lugha, hawa hapa waponya Kiungu, hapa tumemwagiwa kila kitu. Mungu apewe shukrani, vimekuja kupitia kundi dogo nyenyekevu liitwalo Wapentekoste. Hebu sisi sote na turudi katika Biblia tena. Na turudini, ndugu, tukayavunje madhehebu yetu, na sote tuwe ndugu mmoja”? Mekanisa yote makubwa yangeliungana pamoja, nini kingalitukia? Ndugu, hata pasingekuwapo na haja ya hospitali nchini leo. Hiyo ni kweli. La, kungelikuwepo na vipawa vikubwa vyenye uwezo mkuu na maajabu yakitendeka miongoni mwa watu, kungekuwepo na heshima nyingi sana, na labda kanisa lingekuwa limekwisha kwenda Nyumbani na ule Utawala wa Miaka Eelfu ungekuwa unaendelea.

¹⁸⁶ Lakini, hata, hawakuliheshimu. Waliwaita watakatifu wanaojifingirisha. Magazeti yalingojea kuwafanyia kila kashfa, jambo chafu ambalo wangeweza kunena, na kuweka kila neno baya na chafu kwake ambalo wangeliveza kunena, na mambo kama hayo, na makanisa walilizomea na kulicheka, na—na kuwadhihaki, na wakawafukuza na kuwazuia wasiingie mijini, na cho chote kile, bila heshima. Sasa, ningeweza kusema mambo mengi sana kuhusu jambo hilo, lakini wakati unaenda sana.

¹⁸⁷ Hebu nije kwenye Maskani ya Branaham, tafadhali. Sasa Mungu ameanza kumwaga vipawa juu yetu. Tunaona jambo hilo. Sasa, kipawa cha Mungu ni nini leo hii? Ni Roho Mtakatifu, ni Roho Mtakatifu aliye ndani yetu. Yatubidi kumheshimu Huyu. Yatubidi kumheshimu juu ya kila mtu aliyemshukia. Yatubidi kutoa... kwa vipawa vya Kiungu vya Mungu. Wakati Yeye anapotuma vipawa hivyo, haidhuru ni vya kweli jinsi gani, havitatusaidia mpaka tufikie mahali ambapo tunaweza kuviheshimu. Mtu fulani anaweza kutoa unabii; kama hauuamini unabii huo, hautakufaidi kitu. Yakubidi uwe na kicho

na yakubidi uuheshimu. Yakubidi kuamini kwamba unatoka kwa Mungu.

¹⁸⁸ Unauamini mpaka uthibitishwe kuwa ni uongo. Ndipo unapothibitishwa kuwa ni uongo, ndipo utakapokuwa na haki ya kutokuuamini, basi usijihusishe nao tena. Lakini mradi umethibitishwa kuwa ni kweli, basi uamini.

¹⁸⁹ Kama mzee Samweli alivyosema siku ile wakati walipotaka mfalme. Alisema, “Nataka kuwaulizeni jambo moja. Niliwahi kuchukua fedha zenu zo zote? Niliwahi kuwaomba riziki? Au, niliwahi kuwaambia jambo lo lote katika Jina la Bwana isipokuwa lilotukia?” Akasema, “Hamhitaji mfalme ye yote, na mfalme wenu hatawafaa kitu.” Naye akawaambia jambo hilo. Akawaletae swali, akasema, “Niliwahi kuwaambia cho chote kama BWANA ASEMA HIVI isipokuwa kilichotukia?”

¹⁹⁰ Sasa, basi watu hawakumheshimu Samweli. “Loo, tunajua, Samweli. Hiyo ni kweli, wewe, hatuwezi kusema kwamba hujatuambia cho chote kilichokuwa sahihi, ila, ila bado tunataka kufanya jinsi *hii*.” Unaona? Haikupasi kutenda jambo hilo. Yakubidi ulitende kwa njia ya Mungu.

¹⁹¹ Tunampokea Roho Mtakatifu, sio kwa kupeana mikono na mchungaji. Kumpokea Roho Mtakatifu ni kumpokea Kristo ndani yako, kwa sababu Yeye ndiye Mjumbe wa Mungu kwa siku ya leo. Roho Mtakatifu ni Mjumbe wa Mungu, na lazima tumheshimu. Ajapo, usiseme, “Ha-ha! Ha-ha! Ha-ha! Tazama mwanamke yule pale akipiga mayowe, na kulia, machozi yanatiririka mashavuni mwake. Tazama mwanamume yule pale, mikono inatikisika naye anatemeka na kulia. Unajua hicho ni nini? Hicho ni msisimko tu wa kujifanya.” Unamkufuru Roho Mtakatifu. Yakubidi kuheshimu jambo Hilo.

¹⁹² Nakumbuka, hapa muda fulani uliopita nilikuwa huko Oregon, mnamo, imekuwa kama miaka kumi na miwili iliyopita. Na wasichana wadogo wawili maripota Wakatoliki wakashuka wakaja. Si kwa sababu walikuwa Wakatoliki, hilo si kitu; kwa sababu nimekuwa na Waprotestanti wengi kama hao, Waprotestanti wengi kuliko nilivyo nao Wakatoliki, wakinidhihaki. Na—na—na kwa hiyo wasichana hawa wakashuka wakaja kutoa ripoti. Kwa hiyo mara walipoingia, niling’amua hiyo roho mara walipoingia, basi nikasema, “Sawa, sasa mnataka kutoa lawama gani mnayoficha sasa?” Ndipo msichana huyu akachomoa sigara na akaanza, nami nikasema, “Usiiwashe hiyo unapokuwa katika chumba changu. Hebu iache tu.”

¹⁹³ Kwa hiyo akaketi pale kidogo, naye akanitazama kana kwamba angeweza kunichunguza namna *hiyo*, naye akaanza kuzungumza kidogo. Akasema, “Vema, nataka kukuuliza maswali machache.”

Nikasema, “Endelea.”

¹⁹⁴ Akasema, “Imekuwaje kwamba wewe una uhusiano na hili kundi la watakatifu wanaojifingirisha juu hapa?” Akasema, “Je! wewe ni mmoja wao?”

Nikasema, “Mimi ni mmoja wao.”

¹⁹⁵ Naye akasema, “Vema, wataka kuniambia kungekuweko na kitu cho chote cha Kiungu kwenye mambo hayo?”

Nikasema, “Sasa, kwa kuwa wewe ni Mkatoliki hutaliamini.”

Akasema, “Unajuaje mimi ni Mkatoliki?”

¹⁹⁶ Nikasema, “Najua u Mkatoliki. Nitakuambia jina lako ni nani, unaona, na wewe u nani.” Hilo lilimstusha sana.

¹⁹⁷ Akasema, “Vema, unataka kuniambia kwamba watu wa namna hiyo wanasema wataishi hapa duniani na wawe kule Mbinguni?” Akasema, “Nisingetaka kuwepo Mbinguni na watu kama hao.”

¹⁹⁸ Nikasema, “Lisikutie wasiwasi sana. Maadamu unafikiria jinsi hiyo, hutakuwepo huko, kwa vyo vyote, unaona.” Nikasema, “Hutakuwa na wasiwasi wo wote kuhusu jambo hilo.”

¹⁹⁹ Nikasimama tu, nikamkazia macho. Na ndu—ndugu wachache walikuwa wameketi jengoni. Nikasema, “Sina hasira. Na-nataka tu kukujulisha unaposimama, unaona.” Kisha nikasema, “Utaandika, unataka kuja hapa kutafuta mambo fulani, nawe hutaandika kamwe kile nilichokwambia. Utajitungia hadithi. Basi nenda zako ukaiandike, lakini nataka kukwambia jambo moja. Wewe andika kashifa yo yote unayotaka kuandika, na,” nikasema, “kabla ya kufa kwako, sauti yangu itaita tena masikioni mwako. Kama haitaita, basi utajua mimi ni nabii wa uongo.” Nikasema, “Sasa, wewe andika tu lo lote unalotaka kuandika, ni shauri yako. Nimekupa uhuru uende ukaandike unalotaka kuandika. Lakini kabla ya kufa, utasikia sauti yangu ikipiga kelele kwenye masikio yako. Haitakufaa kitu.” Nikasema, “Basi endelea uandike unalotaka kuandika.”

²⁰⁰ Akasimama pale kidogo. Akasema, “Vema, wasemaje kuhusu kundi lile pumbavu juu kule, lililokuwa linapaza sauti na kufanya yasiyofaa usiku uliopita?”

Nikasema, “Wote ni Wakristo.”

“Ati Wakristo?”

²⁰¹ Nikasema “Hakika, wao ni Wakristo.” Nikasema, “Ni Wakristo, wamejazwa Roho Mtakatifu.”

Naye akasema, “Huyo si Roho Mtakatifu.”

²⁰² Nikasema, “Ni kitu gani ungeita Roho Mtakatifu?” Nione angesemaje kuhusu jambo hilo. Nikasema, “Ningetaka kukwambia kitu fulani.”

203 Akasema, “Naam, singetaka kujihusisha na kundi kama hilo.”

204 Nikasema “Sidhani kuna hatari kubwa,” nikasema, “ya wewe kujihusisha namna hiyo.” Nikasema, “Kwa sababu, kama umeshawahi kujihusisha na Mungu au na ye yote wa watakatifu, ungejihusisha namna hiyo.”

Akasema, “Watakatifu wa Biblia?”

205 Nikasema, “Ndio.” Nikasema, “‘Bikira Mariamu’ wenu, mnavyomwita, ambaye ni mungu wenu mke,” nikasema, “kabla ya Mungu kumruhusu aje Mbinguni, ilimbidi kwenda kwenye Siku ya Pentekoste na kumpokea Roho Mtakatifu, naye akapepesuka chini ya Uweza wa Mungu kama mwanamke aliyelewa.”

Akasema, “Huo ni uongo.”

206 Nikasema, “Hebu tulia kidogo.” Nikakifungua Kitabu hapa nikasema, “Tazama hapa,” akageuka. Nikasema, “Hili papa hapa kwenye Kitabu.” Naye akageuza kichwa chake. Nikasema, “Huna hata ujasiri wa kusoma Neno la Mungu.” Unaona? Nikasema, “Hakika.” Unaona, kutokuheshimu. Nikasema, “Sasa unaweza kuondoa pakiti yako ya sigara hapo mezani, uende zako utakapokuwa tayari.” Lakini nikasema, “Nataka ujue jambo moja. Wewe andika lo lote unalotaka kuandika, lakini ukumbuke maneno ya mwisho niliyosema, ‘Katika Jina la Bwana, utayakumbuka kabla hujafa.’” Hakuandika cho chote. Hiyo ni kweli. Aliachana nayo.

207 Ni nini? Kutokuheshimu, akijaribu kudhihaki, akifanya jambo fulani, hawajui watendayo. Sawa.

208 Lakini hapa maskanini, tunawatakeni ninyi nyote kujua mambo haya hapa. Mungu aanzapo kumwaga Roho Mtakatifu juu ya watu, wakati mwingine najua nimewaona watu wakiingia katika mwili walipokuwa—walipokuwa chini ya upako wa Roho, nimewaona wakipita kiasi cha mambo, lakini usiseme cho chote juu yake. Wewe liheshimu, inamisha kichwa chako. Unaweza usilielewe, wala hata mimi, lakini ninataka kuliheshimu, kwa vyo vyote. Sasa lazima tumheshimu Mungu. Na Mungu anapomwaga Roho Mtakatifu, ninashukuru tu, nasema, “Asante, Baba wa Mbinguni. Unatenda jambo fulani kwa ajili ya mtu huyo mpendwa ambaye anataka kuja Nyumbani Kwako kama ninavyotaka siku moja.”

209 Nami ninamwona mtu, kama hapa wakati mmoja ndugu ambaye yuko katika huduma alisema kwamba nilizungumza habari zake. Nasi tulikwenda na kuchukua kanda zote na kumpelekea. Ilikuwa Ndugu A. A. Allen. Naye alisema nilimdhihaki kuzungumzia kuhusu damu ikitoka mkononi mwako na—na kuita jambo hilo thibitisho la kwanza la Roho Mtakatifu, na—nami naamini ilikuwa ni damu na mafuta yakitoka mikononi mwake na paji la uso wake, na kadhalika.

Akasema kwamba hilo lilikuwa—ilikuwa kwamba nilidhihaki jambo hilo na kumwambia kwamba lilikuwa ni la Ibilisi. Nikajibu, nikamwandikia barua, nikasema, “Ndugu Allen.” Akaandika kitini nanyi m—mlikisoma, “Mpendwa Ndugu Branham.” Unaona? Na kwa hiyo basi akatawanya vitini nchi nzima, badala ya kuja na kuniona kuhusu jambo hilo, alifanya hivyo.

²¹⁰ Lakini sasa hili ndilo nililosema, nilisema, “Nitachukua siku zote sita usiku huko Phoenix, na kukupelekea kanda zangu na kukuonyesha.” Jambo ambalo Leo na hao wengine walitenda, na wakawatumia kanda. Nikasema, “Ni wakati mmoja tu jina lako lilitajwa. Watu wakaweka katika dawati langu, wakasema, ‘Ndugu Branham, Ndugu Allen ndiyo kwanza amekuwa mjini na kutuambia kwamba “dalili ya kwanza ya Roho Mtakatifu ilikuwa ni kutoka damu mikononi na kutoka damu usoni, huku mafuta yanatoka katika mikono yako, hiyo ndiyo iliyokuwa dalili ya kwanza.”’”

²¹¹ Nikasema, “Mimi sikubaliani na Ndugu Allen juu ya hayo kuwa dalili ya kwanza ya Roho Mtakatifu, sababu hapana mahali po pote katika Biblia ambapo waliwahi kutokwa na damu mikononi, na—na kutokwa na mafuta usoni na mikononi mwao, kuthibitisha walikuwa na Roho Mtakatifu.” Nikasema, “Roho Mtakatifu alikuwa ni Nguvu ya Mungu katika maisha yao.” Na Yesu alisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waamionio,’ unaona. ‘Katika Jina Langu watatoa pepo,’ na kadhalika. Lakini nilisema, “Hapa kuna jambo moja ningesema kumhusu Ndugu Allen, yeye ni mtu mkuu wa Mungu. Na kama ningeweza kuhubiri vizuri kama Ndugu Allen alivyoweza, singekuwa na ibada ya kuponya, ningehubiri tu Injili.”

²¹² Basi, unaona, baada ya kutawanya makaratasi yale na kila kitu, kwamba mimi “nilifanya hivyo,” kwa kusikiza tu aliyosema mtu mwingine. Lakini hata kama sikubaliani na yule ndugu juu ya nadharia yake, hakika singetaka kumkufuru yule ndugu.

²¹³ Na halafu nikisimama papo hapo, hapa Minnesota, usiku ule huko Minneapolis, Minnesota, na kulikuwako katika kanisa lile kuu, hekalu, pamoja na Gordon Peterson. Na mtu huyu aliyeandika kitabu kile dhidi ya A. A. Allen, na kusema kila kitu kumhusu yeye ambacho kingeweza kusemwa, kisha kasema, “Hata alikuwa na ujasiri wa kuandika kitabu kile cha *Pepo Waumao*, juu ya mwanamke yule, alionyesha alama mikononi mwake ambapo pepo alimuuma, na mambo kama hayo.” Sasa mimi—mimi kwa hakika... (Sijui kama hilo lingeweza kuwa kweli au la, kwa sababu ibilisi ni roho, unaona; lakini mwanamke huyu alidai ibilisi mkubwa mwenye manyoya alikuja na kumuuma kila mahali mikononi na usoni, na kadhalika.) Naye akasema, “A. A. Allen aliandika kitabu hicho.” Na huyo mtu aliyeandika kile kitabu, aliandika makala nzuri juu yangu mimi, na hapa alikuwa ameketi papo hapo katika mkutano

usiku ule (wakati Ndugu Peterson na hao wengine walikuja kuniambia, ameketi hapo) naye alikuwa ananisifu, na kumtweza A. A. Allen.

Nikawaza, “Huu ndio wakati ninaoweza kumtetea Ndugu Allen.”

²¹⁴ Kwa hiyo nilitoka nikaenda pale, nikasema, “Nilikuwa ninasoma hapa makala katika gazeti leo kwamba mtu fulani huyu ambaye yuko mjini, bila . . .” Nikijua yeye alikuwa ameketi pale. Nikasema, “Akisema hapa kwamba A. A. Allen, na lawama hizo zote.” Nikasema, “Ingawa ninathamini sifa alizonipa mtu huyo hivyo,” nikasema, “kwamba sitafuti fedha na mambo kama hayo, na eti niliendesha mikutano minyofu zaidi ya wote hao, na kadhalika, mambo mazuri aliyoyasema.” Nikasema, “Ninathamini hayo. Lakini kama mtu yule ambaye aliandika makala hii hapa gazetini, hakuhakikisha maandishi yake kwa makini kuliko kusema A. A. Allen aliandika hiki *Kuuma Kwa Pepo*. A. A. Allen hakuandika kitabu kile kamwe. Namjua mtu aliyekiandika.” Nikasema, “Hakuandika kitabu kile kamwe. Na kama mtu yule hakuhakikisha makala yake kwa makini sana kuliko hivyo, ninatilia shaka mambo mengine ambayo aliwahi kusema kuhusu Ndugu Allen kuwa ni kweli.” Nikimtetea Ndugu Allen. Nami nikasema, “Isitoshe, kama Ndugu Allen angekosea, afadhali nikutwe kwenye Hukumu nikimuunga mkono Ndugu Allen akiwa amekosea, wakati anajaribu kuwavuta watu kwa Kristo, kuliko kuyalaumu anayojaribu kufanya mtu huyo.” Amina. Hiyo ni kweli. Ndiyo, bwana.

²¹⁵ Ye yote ambaye analiitia Jina la Yesu Kristo, mimi niko pamoja naye kama yeye ni Mprotestanti, Mkatoliki au cho chote kile. Mimi—mimi naweza nisikubaliane naye katika theolojia, bali nataka kumheshimu kama mtumishi wa Kristo na kama ndugu yangu. Unaona? Na haidhuru anafanya kitu gani, yatupasa kumpa heshima Roho Mtakatifu. Sawa kabisa. Ndiyo, bwana. Na tutendapo jambo hilo, basi Mungu atamwaga baraka Zake miongoni mwetu. Sisi tu kundi dogo papa hapa, kama watu hamsini au sitini, au pengine watu sabini na watano wanaoketi hapa ndani usiku wa leo, kama tu, wote pamoja, tungeliungana pamoja na kutoa heshima za kiungu kwa Mungu na kwa Roho Mtakatifu, na kwa yale anayotenda Yeye katika siku hii, na tuheshimu kila kipawa na kila huduma ambayo Yeye anatuma katikati yetu, Mungu ataendelea tu kumwaga Roho Wake juu yetu nasi tutazidi kuwa wengi na kuongezeka. Hamuamini hivyo? Hakika. Yatubidi kumheshimu Mungu.

²¹⁶ Na tuinamishe vichwa vyetu kidogo kwa maombi. Kabla ya kuingia katika maombi, ningetaka kujua kama kuna ye yote ndani humu angetaka kusema, “Ndugu Branham, nataka wewe uniombee, kwamba nitakuwa na heshima kubwa kwa Mungu, kwamba sikuzote nitaweza kufumba kinywa changu dhidi ya mambo ya Mungu, haidhuru ni mambo gani, Mungu

na aweke moyoni mwangu kuheshimu kila kipawa cha Kiungu anachotuma kanisani.” Tafadhali inueni mikono yenu juu, na kusema, “Niombee.” Mungu awabariki. Karibu kila mkono kanisani, nami nilinyosha wangu pia.

²¹⁷ Mungu, nisaidie kuwa mtumishi Wako. Nisaidie kuwaheshimu ndugu zangu, nisaidie kuwaheshimu dada zangu. Na kila Roho wa Mungu anayekuja mkutanoni, kama ni kunena kwa lugha, kama ni kufasiri lugha, kama ni unabii, kama ni vipawa vya upambanuzi, cho chote kile, nasema, “Ee Bwana Yesu, vitume. Vitume, Ee Bwana. Nimejawa na shukurani Kwako.”

²¹⁸ Sasa, Baba wa Mbinguni, tunajua kwamba Wewe u Mungu mkuu na wa kutisha. Tunajua kwamba hasira Yako inatisha mara unapokasirika, mbona, ni—ni jambo la kutisha hasira ya Mungu inaweza kuharibu ulimwengu katika sekunde moja. Lakini Wewe unapotazama chini juu ya Damu ya Bwana Yesu, ndipo hasira Yako inapita. Loo, nifiche katika ule Mwamba wa Kale! Bwana Mungu, ifunike nafsi yangu kwa Damu ya Bwana Yesu. Si yangu tu, Bwana, lakini wale walio humu ndani, pia, usiku wa leo. Tunakupenda, Bwana. Na kila kipawa ambacho Wewe umetupa, ingawa wanaweza kutuita cho chote wanachotaka, Bwana, hilo bado halita...sitaki kuhusiana jambo moja nalo, bado tunakuheshimu Wewe, Mtu aliye mkuu, Roho Mtakatifu aliye mkuu. Tunakupenda, Baba.

²¹⁹ Tunakushukuru Wewe kwa kipawa cha kuponya miongoni mwetu. Tunakushukuru Wewe kwa kipawa cha unabii miongoni mwetu. Tunakushukuru Wewe kwa kipawa cha lugha, na kipawa cha kufasiri. Pia, Ee Mungu, tunaomba kwamba Wewe utaendelea kutuma vipawa miongoni mwetu, vipawa vya Roho Mtakatifu aliye mkuu. Zaidi ya mambo yote, Bwana, uthamini mkuu kuliko wote tulio nao moyoni mwetu ni kwa kile Kipawa kitoshelezacho kabisa, cha Yesu Kristo. Tunakushukuru Wewe kwa neema Yake na rehema Yake, Ambaye anafanya mambo yote haya madogo yawe haki yetu kwa kuteswa Kwake badala yetu na kutoka damu pale Kalvari. Huwatakaswa watu wa kawaida ambao humsikiliza Yeye kwa furaha.

²²⁰ Pia, Bwana, tuna furaha sana kwamba Wewe huja kwa ajili ya watu wa kawaida. Katika Biblia, katika Kitabu cha Luka Mt., tunasoma kwamba, “Watu wa kawaida walimsikiliza kwa furaha.” Leo wanasema, “Loo, hilo ni kundi la watu wa kawaida tu.” Lakini, Bwana, hilo ndilo kundi ambalo lilikusikia Wewe ulipokuwepo hapa katika mwili. Watu wa kawaida walikusikiliza Wewe kwa furaha. Wenye kiburi, matajiri, na wengi wa hao watu wasingekusikiza Wewe. Wafalme, watawala, makasisi wa wakati ule, wasingekusikiza Wewe. Lakini watu wa kawaida walikupokea Wewe kwa furaha.

²²¹ Na, Baba, usiku wa leo, sisi ni watu wa kawaida, nasi tunakupokea Wewe kwa furaha. Tunafuraha kama wao walivyokuwa wakati waliporudi wakifurahi, na wakifikiri lilikuwa jambo nzuri sana, na wenye furaha kwa sababu waliweza kustahimili shutuma za Jina Lake, walipowashutumu na kuwaita kila kitu. Nao walikuwa na furaha sana, kwa sababu ilikuwa ni heshima kwao kuteswa kwa ajili ya Jina la Yesu Kristo. Baba, Mungu, tunaungana pamoja na hao wanafunzi wa siku zile, na kusema, “Tuna furaha.”

²²² Ninasimama usiku wa leo kama Mtakatifu Paulo wa zamani, aliposimama mbele ya Agripa, akasema, “Kwa njia ile ambayo inaitwa uzushi, wazimu, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu.”

²²³ Na wakati Agripa aliposema, “Paulo, kusoma kwingi kumekufanya mwenda wazimu.”

Akasema, “Mimi sina wazimu, Agripa.”

²²⁴ Na halafu hatimaye akafikia mahali, akasema, “Wewe karibu unishawishi mimi kuwa Mkristo.”

²²⁵ Akasema, “Ningependa kwamba wewe ungekuwa kama nilivyo mimi, ila bila ya minyororo hii na vifungo hivi.”

²²⁶ Ee Mungu, ni pendo jinsi gani alilokuwa nalo Paulo, yeye alisema heri angelaaniwa, watu wake wapate kuokolewa. Ee Baba, Mungu, tupe upendo mmoja kwa mwingine kama huo. Tupe huo upendo usiokufa, ule uungwana, ile heshima ya sisi kwa sisi, tuwe Wakristo vya kutosha kutoangalia makosa ya wengine, kutoangalia. Kwa sababu mtu fulani amekwisha barikiwa na Mungu; na anaweza kufanya kosa. Ee Baba, hebu na tusingalie kosa lile, tukijua kwamba huyo ni ndugu mpendwa ambaye labda Shetani alimnasa katika jambo fulani. Lakini kama alikosea, tunaomba, Bwana, kwamba Wewe utamsaidia mwanamume huyo au mwanamke huyo kutoka mahali hapo, kwamba tutakuwa na upendo mioyoni mwetu kumwendea kondoo aliyepotea na kumrudisha kwenye kundi. Lijalie, Bwana. Tusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe wale wanaotukosea. Tujalie, Bwana. Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu. Kwa kuwa ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

[Ndugu Neville anatoa ujumbe wa unabii—Mh.]

²²⁷ Asante, Bwana. Asante Baba. Tunakusifu Wewe, Ee Mtakatifu. Jinsi Wewe ulivyo mtukufu, Baba. Jinsi tunavyokushukuru Wewe, Bwana! Ni faraja jinsi gani kusikia Uwepo wa Roho Mtakatifu na kumsikia Yeye akinena kupitia midomo ya binadamu, kwetu sisi, akithibitisha kwamba Yeye bado yungali Mungu, na yu miongoni mwetu. Tunakushukuru Wewe kwa jambo hili, Baba. Endelea pamoja nasi, Bwana. Tuvumilie, tupate kuwa watu Wako. Tunaliomba kwa Yesu Kristo. Amina.

²²⁸ Je! si ni vizuri sana kuwa Mkristo? Je! si ni vizuri mno kumjua Mungu na kujua Uwepo Wake? Kufikiria ya leo sasa, jinsi Yeye ametenda jambo hili hata kwa mara ya pili. Leo Yeye—Yeye alinena kwa dada hapa, akaja kwenye Nuru ile kama Yeye alivyotenda, ndipo akanena nao kwa sababu wameamini Ujumbe. Yeye yuna utukufu, sivyo? Hamupendi? Wangapi wanampenda Yeye kwa mioyo yao yote, kwa nafsi zenu zote? Yeye ni wa ajabu. Sasa hebu na tusimame, tunapimba wimbo ule mzuri wa kale tunaoupenda sote.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

²²⁹ Loo Yeye si wa ajabu? Wa ajabu! Sasa, kumbukeni ibada Jumatano usiku. Halafu, Bwana akipenda, nitakuwepo hapa Jumapili tena. Bwana akipenda. Tuombeeni juma hili. Tuinamishapo vichwa vyetu katika maombi, nitamwomba Ndugu Neville, mchungaji wetu, kama atakuja kwa ajili ya maneno ya mwisho atakayowapeni. 

HESHIMA SWA61-1015E

(Respects)

Ujumbe huu wa Ndugu William Marrion Branham, uliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Oktoba 15, 1961, katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali ulitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org